# Nipashe

Ijumaa Machi 1, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com

0745 700710
LIKE & FOLLOW US

ISSN 0856 • Na. 0581602

www.ippmedia.com


MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital




UKURASA 21

**BARCA YAJITOSA KWA DE GEA**



# Kwaheri Mzee Rukhsa

- **Kuzikwa** kesho Unguja; pata undani wa safari ya maisha yake... *Ukurasa 7&8*



**Mke** na mume wapigana usiku, nyumba yaungua, wote wafia ndani

UKURASA 5



## Familia yadai polisi fuvu kwa miezi 6

UKURASA 2

# Chama Madaktari chaunga mkono vitita vipya NHIF



- **Hospitali** binafsi zawakataa rasmi wagonjwa kuanzia leo... *Endelea ukurasa 3*






## Rubani asilimua alivyopambana angani shida ya ndege ya ATCL

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA, AL AHLY MOTO UTAWAKA CAIRO** UK.24 **KABWELA** UK.7

# Familia yadai polisi fuvu lao lililoshikiliwa kwa miezi sita

**Na Vitus Audax**

FAMILIA ya Suzani Elias anayedaiwa kukatwakatwa vipande na mume wake kisha kufukiwa katika chumba walichokuwa wanalala, Mtaa wa Nyamhimbi, wilayani Bariadi, mkoani Simiyu, imeibuka na kudai mabaki ya mwili wa mtoto wao likiwamo fuvu ili ikazike.

Hatua hiyo imekuja baada ya familia hiyo kudai kuwa vipimo vya vinasaba vya mwili huo vinaendelea kucheleweshwa.

Ombi hilo limetolewa baada ya miezi sita kupita tangu kukamatwa kwa mume wa marehemu, Juma Peter, anayedaiwa kufanya ukatili huo kisha kuuza eneo lilikuwa na nyumba ya tope na kuhamia sehemu nyingine.

Baba mkubwa wa marehemu, Castory Luhamba, alitoa ombi hilo juzi mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda, wakati akisikiliza na kutatua kero za wananchi wa eneo hilo.

"Binti yetu aliolewa tangu mwaka 2001. Baada ya kuolewa alikuwa kwenye kikundi cha ngoma lakini alikatwakatwa vipande vitatu na kuzikwa kwenye hiyo nyumba. Tumetumia muda mrefu kumtafuta tukidhani kuwa bado yuko hai," alisema Luhamba.

Pia alisema baada ya kufuatilia ilibainika mwili wake ulikutwa katika eneo ulipokuwa ukijengwa msingi na baada ya kufuatilia kwenye uongozi wa serikali, ilitakiwa vipimwe vinasaba ili kuthibitisha kuwa ni mtoto wao.

"Alipelekwa Bugando na wao wakapeleka mabaki hayo Muhimbili na mpaka sasa ni zaidi ya miezi sita hatujapata taarifa yoyote kuhusu vipimo na fuvu liko ofisi za wilaya tunalitaka tuzike binti yetu," alisisitiza Luhamba.

Baada ya maelezo hayo, Dk. Nawanda alisema vipimo vya DNA vilishindwa kufanyika ipasavyo kutokana na mabaki hayo kushikwa na watu wengi kabla hayajapelekwa kwenye vipimo husika, hivyo kusababisha vipimo kurudiwa.

"Tunachokisubiri kwa sasa ni taarifa kutoka kwa mkemia mkuu. Hayo mengine tunaomba mtuachie sisi na majibu yakiwa tayari taratibu zingine zitaruhusiwa kuendelea," alisema Dk. Nawanda.

Septemba 5, mwaka jana, Nipashe ilipoti kupatikana kwa fuvu na mabaki ya binti huyo vilivyobainika baada ya mtu aliyeuziwa eneo hilo kuanza ujenzi na mafundi waliyaona wakati wakiendelea kuchimba msingi ndipo wakatoa taarifa kwa fundi mkuu aliyemjulisha mmiliki wa eneo.

Baada ya mmiliki kubaini, alitoa taarifa kwa viongozi wa mtaa waliotoa taarifa kituo cha polisi na mtuhumiwa kukamatwa na uchunguzi wa mabaki hayo kuanza mara moja.

Taarifa za awali kutoka kwa wataalam wa afya zilieleza kuwa mabaki hayo yana zaidi ya mwaka mmoja tangu yafukiwe ardhini.




Mkandarasi akiendelea na maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi ya mwendokasi katika barabara ya Sam Nujoma, Dar as Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rubani wa ATCL asimulia alivyoamua kuzima injini na kurejesha ndege Dar

**Na Mwandishi Wetu**

RUBANI wa ndege ya Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) Airbus A220-300 iliyopata hitilafu ya injini angani ikiwa njiani kwenda Mbeya, William Zelothe, ameelezea alivyochukua uamuzi wa kugeuza ndege na kurejea Dar es Salaam.

Februari 24, mwaka huu, majira yaa saa 12:00 asubuhi, ndege hiyo iliruka kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Dar es Salaam kwenda Mbeya. Nusu saa badaye ,ikiwa usawa wa Mbuga ya Taifa ya Mikumi mkoani Morogoro, moja ya injini zake ilipata hitilafu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Zelothe alisema hatua za kiusalama alizochukua na wahudumu wa ndege, kutokana na hitilafu hiyo, ni matunda ya mafunzo waliyopewa na shirika hilo.

Siku hiyo, alisema injini ilipata joto na kuanza kutoa moshi ambao uliingia kwenye mfumo wa kiyoyozi (air condition) hali ambayo ilisababisha woga kwa baadhi ya abiria ingawa hakukuwa na taharuki kubwa.

"Moshi uliendelea kwa dakika tano tu ukaisha na wahudumu wetu ndani ya ndege walichukua hatua za kwanza za kiusalama ikiwamo kuwapa taarifa abiria kinachoendelea," alisema.

Zelothe alisema hatua ya kwanza aliyochukua ni kuzima injini iliyokuwa na hitilafu ili kuepusha madhara ambayo yangetokea iwapo hali hiyo ingeendelea kwa muda.

"Kwa kawaida ndege hiyo ingeweza kuendelea na safari hadi Mbeya kwa kutumia injini moja bila shida yoyote lakini kwa kuzingatia zaidi suala la usalama, mimi rubani kiongozi niliona ni busara kuirudisha ndege Dar es Salaam," alisema.

Alisema marubani, wahudumu na wahandisi wa ndege wa ATCL wamekuwa wakipewa mafunzo ndani na nje ya nchi namna ya kukabiliana na dharura wakati wa safari.

"Ndege zote huwa zinatengenezwa na kitu kinaitwa 'redundancy' ndiyo maana zinatengenezwa injini mbili. Moja ikifa nyingine inakuwa na uwezo wa kumaliza safari iliyobaki salama. Kwa hiyo wananchi wafahamu kwamba ndege zetu za Airbus ziko salama, hivyo hakuna haja ya kuwa na hofu," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Ladislaus Matindi, alisema moja ya injini za ndege hiyo ilikuwa imetoka kwenye matengenezo Ujerumani na ilipata hitilafu ya kiufundi angani ikiwa na abiria 122 na hakuna madhara yoyote yaliyotokea.

Alisema ndege hiyo ilipaa Ferbruari 24, saa 12:00 asubuhi na baada ya nusu saa, ilisikika harufu ya moshi ambao baadaye ulitanda ndani ya ndege kutokana na hitilafu kwenye moja ya injini.

Kutokana na hitilafu hiyo, alisema rubani aliamua kurudi Dar es Salaam na baada ya ndege hiyo kufika, abiria 104 walikubali kusafiri kwa kutumia ndege nyingine ya shirika lakini wengine 18 waliomba kubadilishiwa siku ya safari.

Mkuu wa Usalama wa ATCL, Emmanuel Twai, alisema hitilafu ni jambo linalotarajiwa kwenye chombo chochote lakini cha msingi ni tahadhari za kiusalama kuzingatiwa muda wote wa safari.

Alisema hatua ya kwanza ya kiusalama aliyochukua rubani ni kurejesha ndege Dar es Salaam ili wahandisi wa ndege wakague tatizo na kulifanyia kazi kabla ya kuanza safari nyingine.

"Hatua aliyochukua rubani ni sahihi kabisa kwa sababu kama wangekwenda Mbeya, huenda isingepata huduma za haraka kama ambavyo ilipata ikiwa hapa Dar es Salaam ambako kuna wahandisi na wataalamu wote," alisema.

Twai alisema si kila hitilafu inayotokea wakati wa safari ya ndege angani inatolewa taaarifa kwa umma na hilo limekuwa likifanyika ili kuondoa taharuki inayoweza kutokea kwenye jamii kuhusu usafiri wa anga.

Aliyekuwa kiongozi wa wahudumu waliokuwa ndani ya ndege hiyo, Mwanaidi Mwanga, alishukuru mafunzo ambayo ATCL wanawapa ndiyo sababu ilipotokea hitilafu hiyo, walitimiza wajibu wao kitaalamu na bila kutetereka.

"Tunamshukuru pia rubani alitwambia tusiwe na wasiwasi atakabiliana na hali hiyo akasema tuendelee na taratibu zetu za kazi ndani ya ndege na kauli hiyo ilitupa moyo wa kufanya kazi kwa weledi na kuwatuliza abiria ambao walianza kupata hofu kubwa," alisema.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya ATCL Ltd, Ladislaus Matindi (w pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ndege ya Airbus A220-300 iliyopata hitilafu ikiwa angani kuelekea Mbeya wiki iliyopita. Wengine ni Kaimu Mkuu wa Usalama wa shirika hilo, Emmanuel Twai (kulia), Mhudumu wa ndege hiyo, Mwanaidi Mwanga (kushoto) na aliyekuwa Rubani wa ndege hiyo, William Zelotte. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Chama cha Madaktari chaunga mkono vitita vipya vya NHIF

**Na Waandishi Wetu**

VITITA vipya vya matibabu vilivyotangazwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) vinaanza kutumika leo, Chama cha Madaktari nchini (MAT) kimeviunga mkono.

MAT wamesema kuwa wanaunga mkono kuanza kutumika vitita hivyo vipya, wakisema wako tayari kutoa huduma kwa wanachama na mfuko huo.

Chama hicho pia kimethibitisha kushirikishwa na kushiriki kutoa mapendekezo yake katika kuboresha upungufu kiliokuwa kinaona ulipaswa kufanyiwa kazi kwa kuboreshwa.

Rais wa chama hicho, Dk. Deus Ndilanha, katika tamko rasmi la MAT jana, alisema chama hicho kinaunga mkono yale yote yaliyopendekezwa na kamati iliyohusika na maboresho ya vitita vya NHIF.

"Kwanza, tunaunga mkono mapendekezo ya kamati na sisi MAT tunaamini kamati ilikuwa huru na imeenda kwenye uhalisia, na kwa msingi huo yale yote ambayo wameyapendekeza tunayaunga mkono," alisema Dk. Ndilanha.

Alisema mapendekezo yote yaliyowasilishwa na chama hicho kwa kamati yalifanyiwa kazi.

"Nitoe pongezi kwa maboresho ambayo mfuko umeyafanya, na ni baada ya mazungumzo. Ninafikiri wananchi wanakumbuka kwamba mwaka jana mwishoni, mfuko ulitoa kitita na ukasema kwamba una mpango wa kufanya maboresho na kitaanza kutumika mwaka huu.

"Sisi kama MAT tulipata hiyo nafasi baada ya Waziri wa Afya kuunda kamati huru ambayo sisi tulipata nafasi tukaenda kupeleka hoja.

"Na kwa kweli kwa asilimia kubwa yale ambayo madaktari walikuwa wanayapigia kelele, kamati iliyachukua na sasa yanakwenda kufanyiwa kazi, kwahiyo sisi kama chama tunapongeza," alisifu.

Kiongozi huyo wa MAT alisema kuwa kwa kuwa kamati ilitoa nafasi ya watu kupeleka maoni pale wanapoona kuna mahali pa kuboresha, wao kama chama wako tayari kufanya hivyo wakati wowote.

**HOSPITALI BINAFSI**

Wakati kukiwa na hoja hizo za MAT, Chama cha Wenye Hospitali Binafsi (APHFTA) kimeendelea kukazia msimamo wake wa kutopokea wagonjwa wenye kadi za NHIF kuanzia leo.

Mwenyekiti wa chama hicho, Dk. Egina Makwabe alitoa tamko hilo jana baada ya kufanyika kikao jijini Dar es Salaam na kutoa azimio hilo.

"Kuanzia saa sita usiku leo (usiku wa kuamkia leo) hospitali binafsi tumeazimia hatupokea mgonjwa mpya mwenye kadi ya NHIF na walioko wodini wenye hali mbaya tutaendelea kuwahudumia ndani ya saa 48.

"Wagonjwa ambao watakuwa hawajapona ndani ya saa 48 tutafanya smooth transition ya kuwapeleka kwenye hospitali ambazo zitakubali kuwapokea wagonjwa hao."

**MKURUGENZI NHIF**

Katika mazungumzo na Kituo cha Redio cha Clouds FM cha jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Benard Konga alisema kitita ni matakwa ya kisheria, kilianzishwa chini ya Sheria ya Bima ya Afya, Sura ya 395, ambamo mnatamkwa suala la kitita.

Alisema sura hiyo inaeleza ni lazima yafanyike mapitio ya mara kwa mara, mara ya mwisho mapitio yalifanyika mwaka 2016.

Konga alisema kuwa kati ya mwaka 2016 na 2023, NHIF ilikuwa wanafanya mabadiliko madogo ili kuendana na uhalisia.

"Mwaka 2020 tulianza kufanya mapitio kwa kiwango kikubwa na Agosti Mosi, mwaka 2022 NHIF ilitoa taarifa kwa watoa huduma wote kwamba wameshatoa mapitio, wako tayari kutekeleza kitita kipya.

Alisema baada ya kutolewa taarifa hiyo, watoa huduma wengi walipinga wakisema hawajashirikishwa katika mchakato, wakaomba kushirikishwa.

"Serikali yetu ni sikivu, Waziri wa Afya aliagiza kuanzishwe machakato wa kuwashirikisha na kuanzia Agosti 2022 tumekuwa na vikao vingi sana vya kujadili, kuboresha kitita.

"Ilipofika Desemba 2023 majadiliano yalimalizika na ilipofika Januari 2024, tukaanza kutekeleza, tukatoa matangazo kwa watoahuduma, lakini wakasema hawajaona majumuisho ya mwisho. Hivyo wanaomba kuyaona," alisema.

Aliongeza: "Waziri wa Afya akasitisha kuanza kwa kitita Januari Mosi, akaamua kuunda kamati huru ya wataalaamu ambayo ilikuwa na kazi ya kupitia mchakato wote uliofanywa na NHIF kisha ije na ushauri. Kamati ikamaliza kisha ikaja na vigezo vya bei."

Konga alisema kumefanyika maboresho kwa kuwa kila siku kunaiobukia magonjwa mapya, pia namna ya kuyatambua, kuyatibu na kuyachunguza.

Akitolea mfano, Konga alisema kuwa mwaka 2016 hapakuwapo ugonjwa wa corona (COVID-19) lakini sasa ugonjwa huo upo, kitita nacho lazima kiwe na ugonjwa huo .

"Tunaangalia huduma zilizopo nchini, tangu mwaka 2016 hadi sasa kuna maboresho mengi sana, vituo vingi vimejengwa hadi ngazi ya chini, madaktari wameongezeka. Je, kitita chako kinawatambua hawa? Kinatambua vituo?" alisema.

Pia alisema gharama za utoaji huduma zinabadilika kila wakati, zinapanda na kushuka, kwamba hivi sasa kuna watoa huduma wa dawa wengi.

Alisema sababu nyingine ni kupunguza malalamiko na kuongeza kiwango cha huduma zinazotolewa pasipo kumwathiri mtoahuduma.

Kadhalika, Konga alisema kuwa kwa watoahuduma, NHIF wameangalia maeneo makubwa manne ikiwamo eneo ambako mwanachama wa NHIF anakwenda kupata huduma kuanzia zahanati hadi hospitali.

Alisema kitita cha mwaka 2016 kilikuwa kinamwangalia daktari bingwa wa macho aliyeko Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na daktari bingwa wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Amana.

Alisema daktari wa Hospitali ya Amana alikuwa analipwa malipo kidogo kulinganisha na daktari wa MNH, ingawa wote wamesoma darasa moja na wanatoa huduma zinazofanana.

Alisema katika kitita kipya, NHIF wanamtambua madaktari kutoka ngazi ya chini kulinganisha na awali kuanzia ngazi ya wilaya.

"Na wao hivi sasa (madaktari wa chini) wataanza kulipwa kwa kiwango sawa na waliopo MNH, hii inaongeza morali na motisha ya kufanya kazi," alisema.

Konga alisema utoaji dawa ni eneo lingine ambalo linaingiza fedha nyingi kwa vituo vya kutolea huduma.

"Tulifanya mapitio, kuna dawa zaidi ya 200 ambazo hazikuwapo lakini tumeziongeza. Sasa tuna dawa kutoka 700 hadi 900, hii ni faida kubwa kwa mwanachana na mtoahuduma.

"Kuna dawa zaidi ya 200 bei zimeongezeka, yaani tulikuwa tunalipa bei ndogo. Kwa mfano, paracetamo tulikuwa tunalipa Sh. 20, sasa hivi tunakwenda kuziongezea bei," alisema.

Alibainisha kuwa kuna dawa ambazo walikuwa wanalipa bei kubwa (NHIF), sasa wanakwenda kuzishusha, zipo za aina 200, akisema hapo ndipo kuna malumbano kati yao na watoahuduma.

Mkurugenzi huyo pia alitaja eneo ambalo nalo wanakwenda kulifanyia mapitio, aina vipimo za 300 na operesheni, baadhi vinakwenda kushushwa bei.

***Imeandaliwa na Beatrice Shayo, Elizabeth Zaya na Joseph Mwendapole**

# 'Wawekezaji changamkieni maeneo maalum EPZ, SEZ'

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Kitengo cha TEHAMA Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA) amewataka wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuchangamkia fursa za uwekezaji katika maeneo maalum ya uzalishaji wa bidhaa ya EPZ na SEZ.

Elias Mshomba amesema fursa hiyo ni muhimu kwao kuchakata bidhaa kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

Wawekezaji wa ndani na wa nje hupata leseni za kuzalisha na kuchakata bidhaa kupitia progamu za EPZ na SEZ kutoka katika mamlaka hiyo.

Mshomba alitoa rai hiyo wakati wa ziara ya kufanya tathmini ya viwanda vilivyo chini ya mamlaka hiyo katika mikoa ya Njombe, Mbeya na Iringa hivi karibuni.

"Kuna fursa kubwa sana katika mikoa kwa wawekezaji wa Ndani na wa nje kuzalisha na kuchakata bidhaa za mazao kwa ajili ya soko la Ndani na nje hivyo kuchangia ukuaji wa Uchumi wa nchi," alisema.

Alisema kuwa kwa sasa mamlaka kupitia programu zake za EPZ na SEZ inazalisha bidhaa ambazo zimekidhi vigezo/viwango vya soko la Marekani, Asia, Ulaya na masoko mengine ndani ya bara la Afrika.

Alisema katika ziara hiyo walitembelea viwanda 10 ambavyo vimepewa leseni na mamlaka ya EPZA na kuona jinsi ambavyo vimepiga hatua kubwa katika uzalishaji na uchakataji bidhaa mbalimbali zikiwamo za mazao.

Baadhi ya bidhaa za mazao zinazozalishwa na kuchakatwa ni pamoja na maparachichi, mkaa wa kisasa na bidhaa mbalimbali za mbao.

Alisema tathmini hiyo imelenga kuboresha kanzidata ya viwanda vilivyopewa leseni na Mamlaka ya EPZA ambavyo vipo zaidi ya viwanda 200 nchini.

Alisisitiza kuwa lengo la kufanyika tathmini hiyo ni kuiwezesha mamlaka kutatua changamoto za wawekezaji na hivyo kufikia lengo lake la kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda ambapo itasaidia kutengeneza ajira, kuongeza ushindani wa mali ghafi za ndani na kuliongezea taifa fedha za kigeni.

Mshomba alisema kuwa moja ya malengo ya Mamlaka ya EPZA ni kutimiza ndoto za Tanzania ya kuifanya kuwa nchi ya viwanda, kuongeza fursa za ajira, kuongeza usindikaji malighafi za ndani pamoja na kuongezea taifa pato la fedha za kigeni.

Sekta ambazo kwa sasa zinapewa kipaumbele na mamlaka hiyo ni za usindikaji wa mazao ya kilimo, ngozi, bidhaa za misitu, vifaa vya teknolojia, usindikaji madini na bidhaa za vyuma.

Serikali imekuwa inaweka msisitizo mkubwa kwa wazalishaji katika sekta ya viwanda kuzalisha na kuchakata bidhaa za mazao ambazo malighafi zake hupatikana nchini, hivyo kuchangia katika upatikanaji soko la mazao ya wakulima na pia kuongeza ajira kwa vijana huku ikichangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi.

HABARI KITAIFA



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoa wa Morogoro, SP Gabriel Chiguma (katikati), akizungumza na madereva waliohitimu mafunzo ya udereva katika chuo cha VETA Kihonda, mjini Morogoro juzi. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa VETA Kanda ya Mashariki, Wilhad Soko na Mkuu wa Chuo cha VETA Kihonda, Theresia Mosha. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Matukio kujiua kisa wivu, ugumu wa maisha yashtua

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

KAMANDA wa Polisi mkoani Songwe ameeleza kufadhaishwa na vitendo vya watu kujiua kwa wivu wa mapenzi na ugumu wa maisha, akisisitiza elimu itolewe kwa jamii ili kuyaepuka.

Theopista Mallya aliwaambia waandishi wa habari mjini hapa jana kuwa jeshi hilo limeendelea kuimarisha ulinzi na usalama kwa kushirikisha na jamii katika kubaini, kuzuia au kutanzua uhalifu kwa kufanya doria, msako na operesheni.

Hata hivyo, alisema kuwa katika utendaji wao, wamebaini kuwapo matukio mengi ya wananchi kujiua kutokana na sababu mbalimbali, hivyo kuna haja kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa jamii ili kuepuka kujiingiza kwenye matukio hayo ya kujiua.

Alisema kuwa Februari 6, mwaka huu, saa tisa alasiri, katika Kijiji cha Igale, Kata ya Iyula wilayani Mbozi, Adam Motela (58) alikutwa amefariki dunia chumbani kwake baada ya kunywa sumu huku mwili wake ukikutwa umelazwa kifudifudi. Ilidaiwa kuwa alichukua uamuzi huo baada ya kunywa pombe kupindukia baada ya kufiwa na mama yake mzazi.

Kamanda huyo alisema mama mzazi wa marehemu huyo alifariki dunia Januari 14, mwaka huu, kifo ambacho kilisababisha msongo wa mawazo, hata kunywa pombe kupitiliza.

Alidai kuwa Motela pia alikunywa sumu ya kuulia magugu aina ya Gramoxsone.

Kamanda Mallya aliongeza kuwa siku ya Februari 10, saa tano asubuhi, katika Mtaa wa Nyerere, Kata ya Chipaka, Halmashauri ya Mji Tunduma, Dotto Mwajombe (20), aliyekuwa anafanya kazi ya kubadilisha fedha za kigeni, alikutwa amefariki dunia, akidaiwa kujinyonga.

Kamanda Mallya alisema kuwa Januari 13, mwaka huu, saa sita usiku, katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi, Dicto Shitindi (35), mkazi wa Kijiji cha Bara, alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu baada ya kunywa dawa ya kuulia magugu aina ya Gramoxone. Alidaiwa kujifungua chumbani na kunywa sumu hiyo. Sababu za uamuzi huo hazijafahamika.

Februari 21, mwaka huu, saa 10 jioni, katika Kitongoji na Kijiji cha Ikinga, Tarafa ya Bundali wilayani Ileje, Victor Chamba (24) alikutwa amefariki dunia chumbani kwake, akidaiwa kujinyonga akitumia kipande cha shuka na uchunguzi ulibaini alikuwa anaugua ugonjwa wa akili.

Februari 22, mwaka huu, saa nne asubuhi, Kenan Mbiye (50), mkazi wa Mtaa wa Kisangani, Kata ya Muungani, Halmashauri ya Tunduma, alikutwa amefariki dunia chumbani kwake kwa kujinyonga akitumia kipande cha waya ya umeme, sababu ikidaiwa msongo wa mawazo.

Ilidaiwa kuwa Mbiye alichukua uamuzi huo baada ya kuachana na mke wake.

Kamanda Mallya pia alisema kuwa Februari 26, saa moja asubuhi, Egnasho Simchimba (18), mkazi wa Kijiji cha Igamba, wilayani Mbozi, ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha nne katika Sekondari ya Shiwinga alikutwa amefariki chumbani kwake baada ya kunywa sumu aina ya Acteric.

Februari 23, mwaka huu, saa mbili usiku, Ibrahim Mbukula (30), mkazi wa Mtaa wa Kiwanda, Kata ya Mlowo, wilayani Mbozi, alikutwa amefariki dunia baada ya kunywa sumu, chanzo kikidaiwa mgogoro wa ndoa wa muda mrefu kati yake na mke wake.

Kamanda Mallya alisema Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Songwe kuacha kujichukulia sheria mkononi kwa kufanya vitendo vyovyote vya kihalifu na kuwasihi viongozi wa dini na kimila kuendelea kutoa elimu kwa jamii kutumia nyumba za ibada na mikutano ya hadhara.

Alisema utoaji elimu hiyo utasaidia kutokomeza janga hilo la watu kujiua, huku akiwataka wananchi pindi wanapopata changamoto za kimaisha wawashirikishe watu wanaowaamini ili kuwasaidia kutatua changamoto zinazowakumba.

## Wanajeshi wa Tanzania wafundishwa Kifaransa

**Na Beatrice Shayo**

ZAIDI ya maofisa 200 wa Jeshi la Tanzania walioko katika misheni za kulinda amani katika maeneo mbalimbali duniani, wamepatiwa mafunzo ya Kifaransa na kutunukiwa stashahada ya Programu ya Lugha ya Kifaransa kupitia Kituo cha Utamaduni cha Alliance Francaise.

Hayo yalibainishwa juzi jioni na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mbarouk Mbarouk.

Alisema serikali inatambua juhudi zinazofanywa na Alliance Francaise ambao wameendelea kuchangia katika kuongeza uandikishaji wanafunzi katika utoaji programu za lugha ya Kifaransa na kuandaa matukio ya kuonyesha utamaduni wa Kifaransa.

"Tunathamini jukumu la Alliance Francaise, imeendelea kutoa madarasa ya lugha ya Kifaransa kwa maofisa wa Jeshi la Tanzania ambao wametumwa katika misheni za kulinda amani katika sehemu mbalimbali za dunia.

"Zaidi ya maofisa 200 wa jeshi wamepitia mafunzo ya Kifaransa na wametunukiwa diploma zao katika madarasa ya lugha ya Kifaransa kupitia kituo hicho. Hii imewasaidia sana katika utekelezaji majukumu yao," alisema.

"Tunatambua juhudi zinazofanywa na kituo cha kitamaduni cha Ufaransa, ambao wameshiriki na wameendelea kuchukua sehemu kubwa katika kuongeza uandikishaji wa wanafunzi katika matoleo ya programu ya lugha ya Kifaransa, kuandaa hafla zinazoonyesha utamaduni wa Ufaransa na pia kutoa aina nyingi za masomo," alisema.

Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, alisema utofauti wa programu ya mwaka huu ya Francophonie unahusishwa moja kwa moja na utofauti wa lugha ya yenyewe kwa watu kujifunza duniani.

"Lugha ya Kifaransa kama lugha ya kimataifa imekuwa chombo cha kuimarisha usalama na kudumisha amani kati ya watu katika kanda na nchi jirani," alisema Hajlaoui.

Pia aliahidi ushirikiano wa ubalozi huo kutokana na serikali kutambua Kifaransa kama lugha rasmi kupitia Shirika la Afrika Mashariki.

Balozi wa Morocco nchini, Zakaria El Goumiri alikiri kasi ya Francophonie kwa ushirikiano wa kielimu na utamaduni, juhudi ambazo jamii imeziona kwa miaka mingi.

# Serikali yajenga soko la kimkakati Tarime

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amekagua na kuweka jiwe la msingi kwenye mradi wa ujenzi wa soko la kimkakati la mjini Tarime unaotarajiwa kugharimu Sh. bilioni 9.6.

Akipokea taarifa ya ujenzi wa soko hilo juzi, Waziri Mkuu alielezwa kwamba mradi huo kwa sasa uko katika hatua ya umaliziaji na umefikia asilimia 82 ya utekelezaji.

Akitoa taarifa ya mradi huo mbele ya Waziri Mkuu, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tarime, Gimbana Ntavyo, alisema shughuli zinazoendelea kwa sasa ni skimming, upakaji rangi, ufungaji milango kwenye maduka na vyoo na ufungaji mifumo ya umeme na maji kwenye jengo kuu la soko.

Alisema kazi nyingine ni uwekaji vigae na terazo kwenye vizimba, maduka ya nje na ndani na kwa upande wa kazi za nje, wanaendelea na uzalishaji wa paving na kuandaa maeneo ya kuzipanga.

"Hadi sasa malipo yaliyofanyika kwa mkandarasi ni Sh. bilioni 5.77 na kwa mshauri ni Sh. milioni 120.36, sawa na asilimia 60.86 ya gharama za mradi.

"Mradi huu utakuwa na maduka 325, vizimba 160, mabucha matatu, migahawa miwili, supermarket moja na benki mbili," alisema.

Akielezea manufaa ya mradi huo, mkurugenzi huyo alisema mradi huo umetoa ajira za muda kwa watu 441 na utakapokamilika, halmashauri inatarajia kuongeza mapato yake ya ndani kwa Sh. milioni 588 kwa mwaka kutokana na mapato yatakayokusanywa.

# Jela miaka mitatu kwa kutoa rushwa mpakani

**Na Joctan Ngelly,**
MISSENYI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Missenyi, mkoani Kagera imemhukumu Rehema Mdaki (46), mkazi wa Shinyanga kutumikia kifungo cha miaka mitatu gerezani au kulipa faini ya Sh. milioni moja baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kutoa hongo ya Sh. milioni nane.

Imethibitishwa mahakamani huko kuwa mshtakiwa alitoa hongo hiyo ili kukomboa mzigo wa dawa za kilimo uliokamatwa kwenye Mpaka wa Tanzania na Uganda wenye thamani ya Sh. milioni 30.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Yohana Myombo baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa pasipo kuacha shaka yoyote.

Hakimu Myombo alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia za kutoa hongo kama yake.

Alisema Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera, Kelvin Murusuri ambaye alipeleka mahakamani mashahidi sita na vielelezo viwili, ulithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu Myombo alisema kuwa siku ya tukio, Agosti 29, 2023 katika Wilaya ya Missenyi, mshtakiwa alikamatwa na fedha za hongo Sh. milioni nane alizokuwa anapeleka kuhonga ili kukomboa mzigo wake wa dawa za kilimo uliokuwa umekamatwa Mei 30, 2023 katika Mpaka wa Mutukula.

Alisema kuwa alikusudia kutumia fedha hizo kuhonga maofisa wa serikali wa Mpaka wa Mutukula ambao ni wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Ofisa Kilimo na Mionzi.

Alisema kuwa kabla hawajapewa hizo, fedha TAKUKURU walipata taarifa na kuingilia mawasiliano kisha kuweka mtego na kumkamata mshtakiwa akitoa hongo ya Sh. milioni nane kupitia kwa ofisa aliyepandikizwa kupokea fedha hizo.

Hakimu Myombo alisema amesikiliza pande zote na kubaini kuwa Upande wa Mashtaka umethibitisha kosa hilo pasi na kuacha shaka yoyote, hivyo mshtakiwa anatiwa hatiani na mahakama.

Upande wa Mashtaka uliomba mahakama itoe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wafanyabiashara ambao wanahonga watumishi wa umma kwa kutaka kupata unafuu na kukwepa kulipa kodi ya serikali.

Wakili Murusuri pia aliomba mahakama itaifishe fedha za hongo Sh. milioni nane zilizokamatwa ili ziwe mali ya umma.

Upande wa Utetezi uliongozwa na Wakili wa Kujitegemea, Geofrey Binamungu ambaye aliomba mahakama impunguzie adhabu mteja wake kwa kuwa ana familia inayomtegemea.

Hakimu Myombo alisema amezingatia maombi ya pande zote mbili na kumhukumu mshtakiwa kutumikia kifungo cha miaka mitatu gerezani au kulipa faini ya Sh. milioni moja ili kuwa fundisho kwa wafanyabiashara wanaokwepa kulipa kodi serikalini na akaridhia maombi ya Upande wa Jamhuri ya kutaka fedha Sh. milioni nane zitaifishwe kuwa mali ya serikali.

Hakimu Myombo alisema mshtakiwa atakwenda gerezani mpaka hapo atakapolipa faini ya Sh. milioni moja na akishindwa kulipa faini atatumikia kifungo cha miaka gerezani.

# Wanandoa wapigana, nyumba yaungua, wote wafia chumbani

**Na Jenifer Gilla**

WATU wawili, mke na mume, wamefariki dunia baada ya nyumba walimokuwa wanaishi kuteketea kwa moto jana katika Mtaa wa Mwongozo, Kata ya Makuburi, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam.

Moto huo unaodaiwa ulianza saa tisa usiku, mbali na kuondoa uhai wa wanandoa hao, pia uliteketeza nyumba na mali zilizokuwamo ndani. Watoto wao wawili wenye umri wa 10 na mitatu.

Kaimu Kamanda wa Jeshi na Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Ilala, Mrakibu Mwandamizi, Elisa Mugisha alithibitisha kutokea moto huo na vifo vya watu hao na kuteketea kwa mali zao.

Alisema walipata taarifa ya moto huo kutoka kwa majirani saa moja asubuhi na kufika eneo la tukio mara moja na kukuta tayari umeenea ndani ya nyumba hiyo, hivyo juhudi za kuokoa wanandoa hao na mali zao zilishindikana.

Alisema nyumba hiyo ilikuwa na vyumba vitano. Kati yake, vitatu viliteketea kabisa na viwili vikiwa na hali mbaya kwa kuwa moto huo uliezua hadi mabati.

Alisema kuwa kwa mujibu wa mashuhuda, wanandoa hao walianza kugombana na kupigana saa tisa usiku. Baada ya ugomvi wa muda mrefu, walisikia kishindo cha gesi kulipuka na kisha moto kuenea ndani ya nyumba.

Alisema chanzo cha moto hakijafahamika. Wanaendelea na uchunguzi. Watatoa taarifa baada ya kubaini chanzo.

Mugisha alishauri jamii kutoa taarifa za majanga ya moto mapema ili kunusuru vifo na upotevu wa mali unaoweza kusababishwa na matukio hayo pale huduma inapochelewa kutolewa.

Mmoja wa mashuhuda ambaye hakutaka jina lake kutajwa gazetini, alidai kuwa walianza kusikia malumbano kisha kupigana majira ya saa 8:15 usiku, lakini hawakuwafuatilia kwa kile alichotamka "ni kawaida yao kupigana".

Alidai kuwa saa tisa usiku alisikia kishindo kisha moto mkubwa ukaanza kuwaka na kusambaa ndani ya nyumba hiyo, hivyo akatoka pamoja na majirani wenziwe kwa ajili ya kutoa msaada kwa watu hao.

Jirani huyo alidai kuwa juhudi za awali za kuwaokoa zilishindikana kwa kuwa mlango ulikuwa umefungwa kwa ndani na hata walipowaita ili kuufungua hawakufanya hivyo.

Alisema watoto wao walinusurika katika tukio hilo kwa kuwa waliamua kwenda nje na kukimbia wakati wazazi wao walipoanza kupigana.

"Tunahisi pengine mmoja wao alidhamiria kulipua gesi kwa sababu walikuwa wameshapigana sana, tulishazoea kuwasikia wakipigana usiku. Kwahiyo, haikutushtua sana na hawa watoto malaika aliwasimamia wakapata akili ya kukimbia kabla moto haujawashwa," alidai.

## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI | ZACHARIA ANTHONY KAPAMA | KIFURU KINYEREZI-ILALA | 14/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 115345, KIWANJA NAMBA 124, KITALU '24' KIBADA KIGAMBONI 2.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1002975 KIWANJA NA. 2483, KITALU 'A' MBEZI MANYEMA 3.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214 KIGOGO KATI 4. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO KINZUDI GOBA | 1.SALUM JUMA NYANDOTO 2. SALUMU JUMA NYANDOTO 3.SALUM JUMA MARWA 4.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.KIBADA- KIGAMBONI 2.MBEZI MANYEMA 3.KIGOGO KATI 4.KINZUDI GOBA | 13/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | LUCAS NTIRUHUNGWA MZYENGE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JAFETH YONA MZAVA | MIKWAMBE- KIGAMBONI | 06/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | HP PLANNERS & EVENTS MANAGEMENT LTD | NYUMBA (2) | 1.JAMES NDASKOI NNKO 2.DAPHROSER ABEID HAMZA | 1.TEGETA 2.KIGAMBONI | 16/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA | KASSIAN ANTHON NINDI | TABATA KISUKULU | 21/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | NYUMBA (2) | 1.HASSAN RAMADHANI HARASHI 2.HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | 1.YOMBO DOVYA-MAKANGARAWE 2.TAMBANI MKURANGA | 14/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | MHINA JOSEPH KWELLA | NYUMBA | MHINA JOSEPH KWELLA | PUGU | 15/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| HEAD OFFICE | CHITEGETSE MONICA MIGEMBE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | CHITEGETSE MONICA MIGEMBE | MBWENI MPIJI-KINONDONI | 18/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MARIAM DARUWESHI IDDI | NYUMBA | MARIAM DARUWESHI IDDI | KIBUGUMO-KIGAMBONI | 19/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 13/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | JOYCE GENES SHIRIMA | NYUMBA | FRIDA ELIESKIA FUE | HONDOGO KIBAMBA | 14/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | DATIVA BATHOLOMEO MALLYA | GARI TOYOTA KRUGER T864 DSQ NA BREVIS T271 DHG | 1.DATIVA BATHOLOMEO MALLYA 2. CAYUS PASSIAN MRINA | SINZA | 18/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | HAFIDH HASSAN HAFIZO | NYUMBA | HAFIDH HASSAN HAFIZO | MWANDEGE- MKURANGA | 13/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | BENJAMIN JOACHIM MUSHI | NYUMBA | JOHN MROSHI MUSHI | KITUNDA ILALA | 18/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | RAJABU MOHAMED MUOMBWA | NYUMBA | RAJABU MOHAMED MUOMBWA | YANGEYANGE-MSONGOLA | 08/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | INNOCENT DIDAS MUMBURI | NYUMBA | KHADIJA SEIF SINKAMBA | VINGUNGUTI- ILALA | 07/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | JUTIA ABDALA SANZE | NYUMBA | JUTIA ABDALLA SANZE | PUGU BOMBANI -ILALA | 08/03/2024 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | SAMSON MUSSA SAMANYI | NYUMBA | ZAKARIA WAMBURA NYAHULE | MAJOHE | 12/03/2024 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | RAMADHANI HATIBU SAUKA | NYUMBA | JANE ELIAS MASALALILA | KITUNDA-ILALA | 13/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | GODFREY JOSEPH MZANJE | NYUMBA | GODFREY JOSEPH MZANJE | MARAMBA MAWILI | 14/03/2024 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | DIANA MORRIS MSECHU | NYUMBA (2) | 1.MOHAMED HUSSEIN MBOWETO 2.DIANA MORRIS MSECHU | 1.MARAMBA MAWILI 2.MAJOHE | 14/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | NYUMBA | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | TEGETA A - GOBA | 20/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | DAVID ABEL MLAU | CHARAMBE -MBAGALA | 19/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 11/03/2024 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 12/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.IGELEGELE BUGARIKA 2. BUJINGWA-MWANZA | 12/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SELEMANI CHARLES MNIKO | NYUMBA | SELEMANI CHARLES MNIKO | MBUGANI -MWANZA | 13/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | LAMECK RICHARD RWEYONGEZA | NYUMBA | LAMECK RICHARD RWEYONGEZA | KIVULE | 11/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | MASUDI JUMANNE RAMADHANI | NYUMBA | BEATRICE STEPHANO KISHERU | SARANGA | 12/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | NASSOR KHALID OTHMAN | NYUMBA | BAHATI SUMBU MTINDYA | MBEZI MAKABE | 12/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | NYUMBA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | UKONGA | 11/03/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | OWDEN MKUMBALA NYONDO | NYUMBA | OWDEN MKUMBALA NYONDO | ISYESYE-MBEYA | 12/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | WILLY MWITIKA MGOGO | NYUMBA | WILLY MWITIKA MGOGO | MLOWO-MBEYA | 20/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 13/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA ZENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 14/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0715868000/0714939933/0785242219/0759282344/0787129539/0767808848/0754497396/0678799566/0655715138**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

217858501

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuna jambo la kujifunza kutoka mradi Bwawa la Julius Nyerere

**FEBRUARI** 25, mwaka huu, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alifanya ziara katika mradi wa kufua umeme wa Bwawa la Julius Nyerere, kwa lengo la kukagua maendeleo ya kazi hiyo.

Ziara hiyo ilijumuisha maofisa waandamizi wa wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, mhandisi Fulcheshmi Mramba, watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) chini ya Mkurugenzi Mtendaji, Mhandisi Boniface Nyamo-Hanga, viongozi wa mkoa wa Pwani wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Abubakar Kunenge, wakuu wa vyombo vya habari, wahariri na waandishi wa habari.

Katika ziara hiyo ambayo pia ilimjumuisha Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ilishuhudiwa mtambo mmoja kati ya tisa ya kuzalisha umeme katika bwawa hilo, wenye megawati 235 ukiwa umewashwa, hivyo kuongeza kiwango cha umeme katika gridi ya taifa.

Hatua hiyo imesaidia kupunguza makali ya mgawo wa umeme yaliyokuwa yakiwakabili wananchi kwa miezi kadhaa. Licha ya kuingizwa kwa kiwango hicho, pia ilishuhudiwa mtambo mwingine ukiwa katika hatua za mwisho za kukamilika, hali itakayowezesha kuingizwa megawati zingine 235 na kuingizwa kwenye gridi na hatimaye tatizo la mgawo au kukatikakatika kwa umeme kuwa historia.

Hiyo ni habari njema kwa kuwa kuwapo nishati hiyo kwa wingi, kutachochea maendeleo ya uchumi katika sekta za uzalishaji na uboreshaji huduma katika miradi ya kijamii kama vile afya, elimu na maji kwa kuwa umeme ni nyenzo muhimu katika kufanikisha azma ya jambo lolote.

Pamoja na furaha inayotokana na kuongezeka kwa umeme katika gridi ya taifa, liko jambo moja ambalo linatoa funzo kubwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ile ya kimkakati. Jambo hilo ni ushirikishaji wa wazawa katika huduma mbalimbali kupitia miradi hiyo, maarufu kama 'local content'.

Katika mradi huo, huduma mbalimbali kama vile ununuzi wa vifaa vinavyotumika katika ujenzi wa bwawa hilo, sare, vyakula na viburudisho wa watumishi na wageni, vilitolewa na kampuni za ndani.

Akijibu moja ya maswali yaliyoulizwa wakati wa ziara hiyo, Mhandisi Mramba alisema suala hilo lilizingatiwa kikamilifu kwa kuwawezesha Watanzania wanaozalisha vifaa vinavyohitajika katika miradi huo pamoja na huduma mbalimbali kupewa kipaumbele. Mhandisi Mramba alibainisha kwamba vifaa kama mabati, saruji na nondo zilizotumika kwenye mradi zilinunuliwa kutoka kwenye viwanda vya ndani.

Alisisitiza kwamba Watanzania walipewa kipaumbele katika utoaji wa huduma mbalimbali kutokana na mahitaji yaliyokuwapo na yaliyopo katika mradi huo unaoendelea kutekelezwa. Pia alisema hata mshauri mwelekezi, alitoka ndani ambaye ni Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kupitia kitengo chake cha ushauri elekezi (TECU). Hata vyakula vinavyotolewa kwenye mradi huo kama vile unga, mchele, samaki na nyama, ni dhahiri vinatolewa na wazabuni wazawa kama ilivyoonekana.

Inatia faraja kuonyesha kwamba wazawa wamepewa kipaumbeke katika utoaji wa huduma kupitia mradi huo, hivyo kunufaika kiuchumi na kijamii, vinginevyo huduma hizo zingetolewa na kampuni za nje hatimaye Watanzania kuachwa kama washangiliaji wa mchezo.

Kutokana na ushirikishwaji huo wa Watanzania katika utoaji wa huduma mbalimbali ikiwamo viwanda vya ndani kupewa nafasi ya kuuza vifaa vyao, ni hatua kubwa kimaendeleo. Kwa kufanya hivyo, wananufaika moja kwa moja kwa kupata zabuni pamoja na kutoa ajira kwa wananchi.

Miaka ya nyuma iliwahi kuelezwa kuwa baadhi ya huduma vikiwamo vyakula zilikuwa zikitolewa na kampuni kutoka nje hali ambayo iliwanyima Watanzania fursa licha ya kuwa na uwezo wa kufanya kazi hizo.

Hivi sasa kuna miradi mbalimbali inayoendelea kama vile ujenzi wa barabara na reli ya kisasa kwenye maeneo mbalimbali, hivyo wahusika katika utekelezaji wa kazi hizo, hawana budi kujifunza kupitia mradi wa Bwawa la Julius Nyerere.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Yasmine Protace

# Kwa hili tunalolishuhudia, tumpatie Mama wa Nchi maua yake ametenda

**KWA** muda wa miaka mitano na siku zaidi ya 114, vyama vya siasa havikuwa na fursa ya kufanya mikutano ya hadhara kama sehemu ya shughuli ya siasa nchini.

Mabadiliko ya uongozi yaliyotokea Machi mwaka 2021 yakifunguka tena kwa shughuli za kisiasa huku vyama vya siasa, vikiwa vimepata nafasi kushiriki kwa dhati.

Ni mambo yaliyomgusa Rais Samia Suluhu Hassan, akaamua kuwatuliza wanasiasa wenzake katika nyendo zao.Kwa kazi yangu ya uandishi, ilinikutanisha na wadau wengi.

Kimsingi, matumaini ya wananchi wa pande zote za kisiasa yalikuwa kuona Rais Samia anafanya wepesi kurudisha mikutano hiyo.

Nakumbuka Rais Samia alimaliza mwaka huo , ikionyesha kipimo chake kingine cha kisiasa, alivyokuwa anatakiwa kukivuka.

Kilikuwa kipimo ambacho Rais Samia alidhihirisha, huku maelfu ya wananchi wa Tanzania wakisubiri tamko la Rais Samia kuhusu shughuli za kisiasa.

Tamko hilo lilikuwa muhimu, huku Katiba ya nchi nayo ikiruhusu kufanya uamuzi kadri anavyoona inafaa kwa maslahi ya nchi.

Rais Samia alivuka wakati na kufanya uamuzi, akihakikisha tamko lake kuhusu shughuli za kisiasa linakuja wakati ambao ameridhishwa na kile alichokipanga.

Uthibitisho wa hilo ni hotuba yake iliyosema "nasimamisha na kufunguga nchi" akiwa amelenga kutekeleza kwanza mikakati iliyokuwa mezani kwake kuhusu marekebisho kadhaa ya masuala ya uongozi nchini.

Alianzia shughuli za diplomasia, afya, uchumi na ziara kadhaa katika nchi za Afrika na nje ya Afrika. Rais Samia akiendelea na shughuli hizo, huku akichora ramani yake ya kisiasa kuhusu namna anavyotaka nchi iendeshwe na wanasiasa wanapaswa kufanya nini kwa maslahi ya wananchi.

Kana kwamba haitoshi, akaadhimisha Siku ya Demokrasia nchini, akiandika makala mazuri ambayo ikaonyesha ramani yake kwenye siasa.

Akafafanua, anahitaji siasa za kistaarabu na wanasiasa wanaweza kuendesha mikutano bila matusi, kuvunjiana heshima na kutupiana kashfa.

Baada ya hapo Rais Samia, akafanya mazungumzo na viongozi wa vyama vya siasa mbalimbali pamoja na kukutana nao kwenye Jukwaa la Vyama, huku akishauriwa kuendelea kuongoza vizuri nchi yetu.

Awamu nyingine, akakutana na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, wakiwa na ajenda kuu ya maridhiano. Katika mikutano yao viongozi hao wawili walikubaliana na kuendesha siasa za kistaarabu kwa maslahi ya nchi.

Katika kipindi hicho ndipo Rais Samia alileta falsafa yake ya R4 yenye kulenga Maridhiano, Amani na Ustaarabu miongoni mwa wadau na viongozi wa kisiasa bila kuwasahau wananchi.

Haijalishi mafanikio ya R4 yamefikia kiasi gani, lakini furaha iliyopo sasa katika mikutano ya hadhara na maandamano yanayofanyika sehemu mbalimbali nchini ni matokeo ya maono ya Rais Samia, kuwaachia watu uhuru wa kujieleza pasipo kutweza haki za wengine.

Kama kiongozi mkuu wa nchi, alijaribu kulinda taswira ya serikali ya Tanzania, kisha akajenga taswira ya hali ya demokrasia. Kwa kipindi cha miaka mitatu, Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kuwaachia uhuru wa kujieleza hali ambayo inawapa furaha wanasiasa na manazi wao.

Baadhi ya vyama hivyo vimekuwa kwenye mchakamchaka wa kisiasa na kuitengeneza taswira ya kidemokrasia kuwa yenye kulinda haki na kuheshimu uhuru wa watu wengine.

Samia naye akafanya hayo, akiruhusu wasaidizi wake ndani ya chama kuhakikisha wanafanya siasa za kistaarabu.

Mambo yanaiva, Paul Makonda wa CCM akizunguka sehemu mbalimbali kuwahutubia wananchi na kusikiliza kero zao na kukiuza vizuri chama chake, hali kadhalika kina Benson Kigaila na wezake wa CHADEMA nao wapo kwenye mikutano na maandamano ya amani kwa kila mkoa. Wako katika majiji wakianzia na Dar es Salaam kisha Mwanza, Mbeya na wiki hii, Arusha.

Hiyo inamuachia Rais Samia taswira kuwa mjenzi wa nuru ya kisiasa inayoendelea nchini. Anaweza kuzungumziwa kwa namna yoyote, lakini walau katika hilo asinyimwe maua yake, kwani ametenda katika siasa za nchini.

Kimsingi ameelekeza, amesimamia, ameonyesha dira, amewapa uhuru wasaidizi wake ndani ya chama huru wa kupambana kisiasa na wanasiasa wa vyama vya upinzani.

Ligine nalitazama, amejaribu kutenganisha shughuli za chama na serikali. Kwamba CCM wanaweza kuendesha hekaheka za siasa kwa 'kunyukana' na wapinzani wao bila serikali kutia mkono wake.

Leo tukianza kumhesabia siku kufikia stendi ya miaka mitatu.

ALI HASSAN MWINYI 1925-2024

# Kwaheri Mzee Rukhsa

**Na Restuta James**



MSIBA mkubwa. Ndivyo ilivyo kutokana na kifo cha Rais mstaafu wa Awamu ya Pili, Alhaj Mzee Ali Hassan Mwinyi, kilichotangazwa kutokea jana Dar es Salaam.

Kifo cha Mzee Mwinyi, maarufu Mzee Rukhsa, kimetangazwa ikiwa ni takriban wiki tatu tangu kutangazwa kifo cha Waziri Mkuu wa zamani, Edward Lowassa, Februari 10, mwaka huu.

Akilitangazia taifa msiba huo kupitia vyombo vya habari jana, Rais Samia Suluhu Hassan alisema Mzee Mwinyi alifariki dunia jana saa 11:30 jioni katika Hospitali ya Emilio Mzena, Kijitonyama, mkoani Dar es Salaam.

Rais Samia alisema Rais mstaafu Mwinyi alikuwa amelazwa katika hospitali hiyo akipatiwa matibabu ya saratani ya mapafu.

Kwa mujibu wa Rais Samia, Mzee Mwinyi alikuwa anapatiwa matibabu tangu Novemba, mwaka jana, jijini London, Uingereza na baadaye kurejea nchini na kuendelea na matibabu hayo katika Hospitali ya Mzena.

"Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki na watanzania wote kwa msiba huu," alisema.

Rais Samia alibainisha kuwa kiongozi huyo mstaafu atazikwa kesho Unguja, Zanzibar na taratibu za mazishi zitatangazwa baadaye.

Kutokana na msiba huo, Rais Samia alitangaza maombolezo ya siku saba na bendera zitapepea nusu mlingoti kuanzia leo.

**HISTORIA YAKE**

Mzee Mwinyi alizaliwa Mei 8, 1925 akiwa mtoto wa Hassan na Asha Sheikh Mwinyi na maisha yake ya ujana aliyatumia akiwa Zanzibar.

Mwinyi alipata elimu ya msingi katika Shule ya Mangapwani, mjini Magharibi, Unguja na baadaye alijiunga na Shule ya Sekondari ya Mikindani Dole, Mkoa wa Mjini Magharibi , Zanzibar.

Alipata stashahada ya elimu ya watu wazima Dublin, Ireland kati ya mwaka 1954 na 1956 na kufundisha katika shule za msingi za Mangapwani na Bumbwini. Pia alisoma na kupata astashahada ya umahiri katika lugha ya Kingereza kutoka Taasisi ya Regent, Uingereza mwaka 1960 na ya umahiri katika Lugha ya Kiarabu, Cairo nchini Misri mwaka 1972 hadi 1974.

Mwinyi alijiunga na Chama cha Afro Shiraz (ASP) mwaka 1964 na kushika nafasi mbalimbali za uongozi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu Zanzibar mwaka 1963. Mwaka 1970, aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mwaka 1977 hadi 1982 alikuwa Balozi wa Tanzania nchini Misri na baadaye kurejea nchini na kuteuliwa mwaka 1982- 1983 kuwa Waziri wa Afya; Mambo ya Ndani ya Nchi na Maliasili na Utalii.

Aliendelea kung'ara katika medani ya siasa mwaka 1984 kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Awamu ya Tatu Zanzibar baada ya hali ya hewa ya kisiasa Zanzibar kuchafuka na kusababisha aliyekuwa Rais wa wakati huo, Alhaj Aboud Jumbe (sasa marehemu), kujiuzulu. Pia aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alimteua kuwa Makamu wa Rais.

Mwaka 1985, alipendekezwa na Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kugombea urais wa Tanzania kutokana na Nyerere kung'atuka na hatimaye kuchaguliwa katika nafasi hiyo kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huo. Alichaguliwa mwaka 1990 katika nafasi hiyo kwa kipindi cha pili cha urais na kutumikia nafasi hiyo hadi mwaka 1995.

Licha ya kuwa Rais wa Tanzania, Mwinyi pia alikuwa Mwenyekiti wa Taifa wa CCM kuanzia mwaka 1990 hadi 1996 alipomwachia kiti Hayati Benjamin Mkapa, ambaye pia alimpisha kiti cha urais mwaka 1995.

**SAFARI ILIVYOKUWA**

Mzee Rukhsa; jiwe la msingi wa mageuzi ya kiuchumi na kijamii, utambulisho wa uongozi wa kuunganisha watu, mwadilifu, mkweli, mnyenyekevu, mvumilivu na mzalendo asiyetiliwa shaka.

Kuna uhusiano wa jina lake la utoto la 'Nzasa' lenye maana ya 'Sikaukiwi' na safari nzima ya maisha yake, kama alivyoeleza kwenye kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', kilichochapishwa mwaka 2020.

Sura ya nne ya kitabu hicho inaeleza hali halisi tangu kuzaliwa kwake hadi kuingia kwenye madaraka makubwa ya kitaifa, akianzia kwenye ualimu hadi Mkuu wa Nchi.

Mwinyi anasimulia katika kitabu hicho kuwa alipozaliwa Mei 8, 1925, alipewa jina la Sihaba ambalo lilikuwa ni shukrani ya baba na mama yake.

Baba yake, Mzee Hassan na mama yake Bi. Asha binti Mwinyi-Shehe, walimpa jina la Sihaba kwa maana ya 'ahsante Mungu kwa kutupatia mtoto wa kiume' ambaye hakuwako kwenye familia yao.

Anasimulia kwamba mtoto Sihaba aliongeza furaha ndani ya familia hiyo, akipendwa si tu na wazazi wake bali na dada zake na akiishi maisha ya kudekezwa kwa kupewa mwanya wa kufanya utundu wote wa kitoto na kuachwa bila kufanywa chochote.

Furaha hiyo bila shaka ndiyo iliyomfanya baba yake ambadilishe jina na kumwita Nzasa (Sikaukiwi) lenye maana ya ardhi oevu au tengefu isiyoishiwa maji.

Hata hivyo, Nzasa ilianzia kwa babu yake mzaa baba, Mzee Mwinyi Magandi, ambaye alikuwa mkazi wa Kijiji cha Kivule, pembezoni mwa barabara kuu itokayo Dar es Salaam hadi Kisiju mkoani Pwani, wilayani Mkuranga.

Mzee Magandi alipewa jina hilo na rafiki zake kutokana na aina ya maisha yake kijijini hapo, akiwa mkulima na mfanyabiashara ndogo, jambo lililomfanya anunue mazao na kuyahifadhi ghalani, hivyo kumfanya awe na chakula cha kutosha mwaka mzima hadi kuwakopesha jirani zake pale wanapohitaji msaada au kununua.

"Matokeo yake, pale msimu wa kilimo ukiwadia, baadhi ya wakulima wenziwe walijikuta hawana chakula wala mbegu. Hao walienda kwa Mzee Nzasa kununua mahitaji yao ambaye badala ya kuwauzia kwa fedha taslimu aliwapa kazi ya kulima mashamba yake kama malipo ya mahitaji yao," anasimulia mrithi wa jina la Nzasa, Rais mstaafu Mwinyi katika kitabu hicho.

Maisha ya raha, furaha na upendo kwa mtoto Nzasa yalidumu kwa miaka minne pekee, kwani baba yake alimhamishia Zanzibar, kwa rafiki yake kwa nia kumfundisha dini ya Kiislamu, akiwa na lengo la kumwezesha Nzasa awe Sheikh mashuhuri baada ya kuhitimu masomo yake ya dini.

Hii ni kwa sababu wakati huo wasomi wakubwa wa dini hiyo ni pamoja na wale waliosoma Chuo cha Ukutani, Unguja. Hili lilimlazimu Mzee Hassan Mwinyi kumpeleka mwanawe Nzasa hadi Mangapwani, kama hatua ya kwanza kuelekea Ukutani.

Katika umri huo wa miaka minne, baba yake alimtaka awe mnyenyekevu, mkarimu, msikivu, mwenye huruma kwa yatima na wazee na asiyeamua mambo muhimu peke yake bila ushauri wa wale anaowaamini.

**SAFARI YA MANGAPWANI**

Nzasa alihamia kwa rafiki wa baba yake, Mzee Swedi bin Mgeni, Mangapwani akiwa na umri huo, japokuwa nia ilikuwa aanze chuo cha Qur'an baada ya kutimiza umri wa miaka saba.

Katika makabidhiano ya mtoto Nzasa, licha ya kumpenda sana mwanawe, Mzee Mwinyi alimpa Mzee Mgeni uhuru wa kumlea na hata alipoanza elimu yake ya dini, ilikuwa ni rukhsa kwa mwalimu wake kumfundisha, kumkaripia, kumwonya, kumkemea na kumchapa.

Alipotimiza miaka saba, mtoto Nzasa alipelekwa chuoni kwa Hayati Maalim Khamis, aliyekuwa mwalimu maarufu wa Qur'an kijijini huko. Kutokana na juhudi yake ya kujifunza, alihitimu masomo hayo ndani ya miezi minne.

Kutokana na kiu yake ya kujifunza, Januari 5, 1933, alifanikiwa kujiunga na elimu ya msingi katika Shule ya Msingi Mangapwani. Hili halikuwa jambo rahisi kwake kutokana na elimu dunia wakati huo kuhusishwa na Ukristo.

Mzee Rukhsa anasimulia kwenye kitabu chake hicho kwamba alifanikiwa kupata nafasi hiyo kutokana na anachokiita "kiherehere" chake cha kutamani shule na hivyo alilazimika kijipitishapitisha ili walimu wamwone waende kuwaomba walezi wake ajiunge darasa la kwanza, baada ya mlezi wake Swedi bin Mgeni, kuridhia.

Pamoja na kwamba shule zote zilikuwa za serikali wakati huo, zilihusishwa na Ukristo, jambo ambalo lilipatiwa ufumbuzi kwa kuruhusu vipindi vya Qur'an na hivyo miaka iliyofuata iliwawezesha watoto wengi wa Kiislamu kujiunga na shule.

Mwaka 1940, Mzee Rukhsa akiwa darasa la nane, serikali ilianzisha mpango wa kujenga chuo kipya cha ualimu, ikilenga kupokea wanafunzi kutoka vijijini, akiwamo yeye.

Hata hivyo, mpango huo ulichelewa kidogo kutokana na vita vya pili vya dunia vilivyokuwa vinaendelea pamoja na mpango wa serikali wakati huo kutaka kusuka upya mfumo wa elimu.

Mwaka 1941, alisoma na kumaliza darasa la tisa wakati akisubiri kujiunga na chuo cha ualimu. Mageuzi ya elimu yalichelewa kutokana na michakato ya ndani ya serikali, lakini hilo halikumkatisha tamaa Mzee Rukhsa kwani mwaka uliofuata aliamua kujisomea darasa la 10 kwa njia ya posta kupitia Rapid Results College ya Uingereza na kuhitimu.

Akajiunga na Chuo cha Ualimu Dole ambako alisoma kwa miaka miwili na mwaka 1945 alirejea Shule ya Mangapwani kama mwalimu, kazi aliyoifanya kwa miaka miwili kabla ya kuhamishiwa kijiji jirani cha Bumbwini, mwaka 1947.

Bumbwini hakukuwa na shule, hivyo alilazimika kuwa kontrakta wa ujenzi wa shule mpya bila malipo huku wanafunzi na wanakijiji wakiwa vibarua; kazi aliyoifanya kwa uaminifu, bidii na maarifa kuhakikisha lengo la kuwafikishia elimu watoto linafanikiwa.

Juhudi na ubunifu akiwa mwalimu wa Bumbwini, zilimpa sifa njema kiasi cha wakaguzi wa elimu kumpongeza na kumpendekeza kwa masomo ya juu zaidi; na mwaka 1954 alipata ufadhili wa kwenda kusomea ualimu Uingereza katika Chuo Kikuu cha Durham, karibu na Jiji la Newcastle. Alifanya kazi kwa miaka mitano na mwaka 1961/62 alifadhiliwa tena kwenda Uingereza katika Chuo Kikuu cha Hull, Leicester kujifunza mbinu za kufundisha ualimu kwa wanafunzi wa ualimu.

Baada ya masomo hayo, mwaka 1962 alirejea Zanzibar na kuteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo cha Ualimu.

# Visa na mikasa ya Mzee Rukhsa ughaibuni

Na Mwandishi Wetu

MIONGONI mwa visa na mikasa aliyokutana nayo Rais Mstaafu wa awamu ya pili, Alhaj Ali Hassan Mwinyi, (Mzee Rukhsa) ni pale alipoona mlango ukifunguka wenyewe siku yake ya kwanza alipofika London kuanza masomo yake.

Mzee Rukhsa anasema katika kitabu chake kuwa alipowasili jijini humo, alifikia katika jengo la Afrika Mashariki (East Africa House), lililokuwa linamilikiwa kwa ubia na nchi za Kenya, Tanganyika, Uganda na Zanzibar.

"Usiku nikapata mshtuko wa kwanza wa kitamaduni. Nilihitaji kwenda haja usiku, nikaamka na kuelekea msalani. Nilipokaribia tu nikaona mlango unafunguka wenyewe. La haula! Mambo gani haya? Kwa mimi niliyeishi Bumbwini nikadhani wachawi wamenifuata," anasimulia katika ukurasa wa 77 wa kitabu hicho.

Baada ya 'kukabiliana' na hofu ya mlango kufunguka wenyewe, kesho yake alielekea chuoni Newcastle, umbali wa kilometa 400 kutoka East Africa House. Kwake ilikuwa nafuu kuondoka kwenye jumba hilo na kuhamia Methodist International House, ili awe karibu na chuo cha Durham, alikokwenda kusoma.

**KUGEUZWA MWANASESERE**

Wakiwa masomoni, baadhi ya familia za wenyeji walikuwa wanaomba wanafunzi hasa wanaotoka nchi za mbali wawatembelee ili kubadilisha mazingira ya chuo; Mwinyi naye alipata bahati hiyo na kwa mara ya kwanza alialikwa katika familia moja iliyokuwa na baba, mama na mtoto aliyekadiriwa kuwa na umri wa miaka mitano hadi saba.

"Basi mtoto yule akaona kama



vile wazazi wake wamemletea mwanasesere. Alinirukia mapajani pangu na kuanza kunipapasa na kuvuta nywele zangu ambazo kwa sababu ya baridi, nilikuwa nimezifuga zikawa ndefu. Sikuwa na raha hata kidogo kwani kichwa chote kiliwaka moto.

"Baada ya chakula nikawashukuru wenyeji wangu na kuwaaga," anasimulia Mzee Rukhsa.

**KUKU MMOJA SIKU 5**

Mzee Mwinyi anasema siku moja akiwa na wanafunzi wenzake wawili, walialikwa na kasisi mmoja kwenda katika jimbo la Lake, lililoko Kaskazini Magharibi mwa London.

"Tukapata mshtuko mwingine wa kitamaduni wakati wa chakula. Mwenyeji wetu alituletea jogoo zima kutoka kwenye oveni (kasoro kichwa na kucha), akaweka mezani.

"Akachukua kisu akakata kwa uangalifu sehemu nyembamba ya nyama ya jogoo yule na kumwekea kila mmoja wetu kipande kwenye sahani yake. Kipande ambacho kilikuwa chembamba kiasi cha kukaribia kuonekana upande wake wa pili.

"Kisha akamwekea kila mmoja wetu kiazi kimoja kikubwa kwenye sahani na mbogamboga kidogo... jogoo aliyesalia aliwekwa kwenye jokofu. Kwa ukataji ule, jogoo huyo tulimla kwa siku zote tano tulizokaa kwenye familia hiyo," anasema.

**APOTEA UK**

Mzee Mwinyi aliwahi kupotea wakati wa likizo yake ya mwisho wa mwaka 1954, kama anavyosimulia mkasa huo kwenye ukurasa wa 80 wa kitabu chake.

Anasema alipomaliza likizo, alikwenda stesheni kukata tiketi ya treni kumrejesha Newcastle, alitoa nauli kama aliyokuwa amelipa alipokuwa anakuja London, bila kujua kwamba nauli zilikuwa zimepanda siku chache zilizopita.

"Wewe husomi magazeti? Imetangazwa katika redio na kuandikwa magazetini kuwa nauli zimepanda. Kusikia vile nilishtuka nikatoa mfukoni mwangu pesa zote nilizokuwa nazo (noti na sarafu) nikamkabidhi (mkata tiketi).

"Yule mzungu akaziangalia kwa dharau... akatumia ncha ya penseli kuzihesabu, alipomaliza akasema fedha zangu hazitoshi.

"Nikamtaka radhi, kwa heshima na taadhima, nikamwomba aniongezee yeye hiyo moja. Akanijibu, hebu angalia nyuma yako uone huo msururu wa watu wanaongoja kukata tiketi, kama kila mmoja akiniomba nimlipie, itanipasa niwe na kiasi gani? Nitaweza?"

Kuona mambo magumu, Mzee Mwinyi akaomba akatiwe tiketi ya fedha aliyotoa ili atakaposhuka akamilishe safari yake kwa mguu. Tiketi yake ilikuwa inaishia kilometa 50, kabla ya kufika Methodist International House, alikokuwa anakwenda.

Kwa bahati, akatokea msamaria mwema (mzungu), ambaye alimwongezea kiasi kilichopungua na akakata tiketi ya safari nzima.

"Lakini huo haukuwa mwisho wa matatizo yangu. Nilipowasili Newcastle likanikuta janga jingine. Kuna umbali kidogo kutoka stesheni hadi Methodist International House, badala ya kufuata barabara kubwa na baridi ile, nikaona bora nifuate njia ya mkato. Kosa! Nikapotea," anasema.

Mzee Rukhsa anasema kuwa baada ya kuhangaika kwa muda, alikutana na kijana mmoja akamwuliza njia ya kufika kwenye hosteli hizo.

"Akaniambia tuongozane mama na yeye anakwenda huko. Nikamshukuru. Njiani akawa ananiuliza maswali mengi sana na mimi nikawa ninamjibu. Mwisho tukawasili Methodist International House, alipohakikisha kuwa nimeona, akaniaga akarudi tulikotoka. Nikamuuliza 'mbona unarudi tulikotoka?' akanijibu 'mimi siendi huko, nilikuwa nakuleta wewe mgeni.' Nikajua kumbe alinionea huruma nisije nikapotea tena," anasilimua.

**ITAENDELEA KESHO**

# Wapewa jukumu mkakati kuacha matumizi fedha taslimu

Na Mwandishi Wetu

WASHINDI 12 wa kampeni ya kuhamasisha matumizi yasiyohusisha fedha taslimu iliyoendeshwa na Benki ya NMB kwa miezi mitatu 'NMB MastaBata – Halipoi' na wenza wao, wamekabidhiwa tiketi za ndege za safari ya kitalii jijini Cape Town, Afrika Kusini (Sauzi) kwa ziara ya siku tano.

Kampeni hiyo ilizinduliwa Oktoba 27, mwaka jana ikiwa na zawadi zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 350. Kwa miezi mitatu, imezalisha jumla ya washindi 1,492, wakiwamo waliojishindia fedha taslimu, ziara ya kitalii Zanzibar na 12 wanaokwenda Afrika Kusini na wenza wao.

Hafla ya makabidhiano ya tiketi kwa washindi hao ilifanyika juzi makao makuu ya NMB jijini Dar es Salaam, wakikabidhiwa na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi, mbele ya Mkuu wa Idara ya Biasahara ya Kadi wa benki hiyo, Philbert Casmir.

Mponzi alisema kampeni hiyo ilikuwa sehemu ya jitihada za benki yake katika kuunga mkono juhudi za serikali kujenga utamaduni chanya miongoni mwa Watanzania wa kufanya matumizi yasiyohusisha fedha taslimu.

"Ilikuwa ni miezi mitatu iliyozalisha washindi 1,492 waliojinyakulia zawadi mbalimbali zenye thamani ya Sh. milioni 350, ambako tulikuwa na washindi wa kila wiki, kila mwezi, papo kwa papo, wa ziara ya utalii Zanzibar na tunahitimisha na hawa wa Afrika Kusini.

"Kupitia NMB MastaBata – Halipoi, tumefundisha wateja wetu na Watanzania utamaduni wa matumizi salama yasiyo ya fedha taslimu, huku tukiwazawadia. Kwamba licha ya kufanya matumizi hayo kwa faida yao, lakini bado NMB ikawawekea washindi zawadi.

"Zawadi zetu katika msimu huu wa tano zilikuwa kubwa na ni kutokana pia na ukubwa wa benki yetu na dhamira tuliyonayo ya kugusa maisha ya walio wengi miongoni mwa watanzania, hususani wateja wetu," alisisitiza Mponzi.

Alibainisha ya kuwa mwisho wa NMB MastaBata ndio mwendelezo wa kampeni nyingine, ambako kwa sasa wanaendelea kutoa zawadi kwa washindi wa kampeni ya 'Weka na Ushinde'.

Mponzi alisema washindi hao 12 na wenzao wakiwa Cape Town, watatembelea 'Table Mountain,' mbuga za wanyama na Kisiwa cha Robben, kuzuru Gereza la Victor-Vorster alikofungwa aliyekuwa Rais wa Kwanza Mzalendo wa Afrika Kusini, Nelson Mandela.

Mkuu wa Idara ya Kadi NMB, Philbert Casmir, alipongeza washindi hao kwa ziara hiyo, huku akiwataka kuwa mabalozi wema wa benki hiyo wakiwa Afrika Kusini na hata kwa jamii ya watanzania punde watakaporejea nchini.

Kwa niaba ya washindi hao walioondoka nchini alfajiri ya jana, Makame Zahoro Ali wa Zanzibar, alishukuru NMB kwa ubunifu uliozaa kampeni hiyo ya NMB MastaBata, inayompa nafasi ambayo hakuwahi kuiota ya kusafiri nje ya nchi kwa gharama za benki hiyo.

"Nilipopigiwa simu kuwa mimi ni mmoja wa washindi wa kampeni hii, nilihisi kama utapeli, lakini baadaye nikapewa maelekezo ya safari na hatimaye nikaamini kwamba safari ipo na ushindi wangu ni wa kweli. Sikutarajia kabisa kusafiri nje ya nchi, ila NMB imefanikisha hili," alisema.

# Jela miaka 10 kwa kuiba ng'ombe, kuwauza Uganda

Na Joctan Ngelly, KAGERA

MAHAKAMA ya Wilaya Missenyi Mkoa wa Kagera imemhukumu Dauson Saimoni (24), mkazi wa Byeju kutumikia kifungo cha miaka 10 gerezani kwa kosa la wizi wa ng'ombe watano wenye thamani ya Sh. milioni 4.4, mali ya Theobati Joseph.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Yohana Myombo baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa pasipo kuacha shaka yoyote.

Hakimu Myombo alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia za wizi.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Inspekta wa Polisi Amoni Lutalibatwa, ulipeleka mahakamani huko mashahidi watano na vielelezo vitatu ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu Myombo alisema kuwa siku ya tukio, Novemba 2, 2023, mshtakiwa huyo aliiba katika Kijiji cha Bubale, Wilaya ya Missenyi na kwenda kuwauza ng'ombe hao Uganda. Alisema kuwa kuna mtu alimwona mshtakiwa akiwa anauza ng'ombe na alipobaini hilo, alimpigia simu kwa mlalamikaji Theobati Joseph kama ulimpa mshtakiwa ng'ombe wake kwenda kuwauza.

Hakimu huyo alisema baada ya kupewa taarifa hizo, mmiliki wa ng'ombe hao alikwenda Kituo cha Polisi nchini Uganda na kutoa taarifa na polisi wa nchi hiyo walifika eneo husika na kukamata mshtakiwa.

Alisema kuwa baada ya mshtakiwa huyo kukamatwa Uganda, mlalamikaji alikwenda Kituo cha Polisi Kyaka, Wilaya ya Missenyi ndipo askari polisi wa kituo hicho walikwenda Uganda na kumchukua mshtakiwa na kumleta katika kituo hicho na alipohojiwa alikiri kuhusika na tukio hilo la wizi wa ng'ombe watano na baada ya upelelezi kukamilika mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani.

Hakimu Myombo alisema amesikiliza pande zote na kubaini kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa hilo pasi na kuacha shaka yoyote, hivyo mahakama inamtia hatiani mshtakiwa kwa kosa hilo.

Mwendesha Mashtaka, Inspekta wa Polisi Amoni Lutalibatwa alidai kutokuwa na kumbukumbu za makosa ya nyuma ya mshtakiwa na kuomba mahakama hiyo itoe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Mshtakiwa huyo alipopewa nafasi ya kuomba kupunguziwa adhabu, alidai hilo ni kosa lake la kwanza, hivyo akaomba mahakama hiyo impunguzie adhabu kwa sababu ana familia inayomtegemea.



# Mil.200/- kurudisha tabasamu kinamama Kata ya Themi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKAZI wa Kata ya Themi jijini Arusha wanatarajia kuondokana na adha ya kufuata huduma ya kujifungulia nje ya eneo hilo, baada ya serikali kupeleka Sh. milioni 200 za kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la mama na mtoto.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usimamizi wa Kituo cha Afya cha Themi, Melace Kinabo, jana alisema kilio cha muda mrefu cha wananchi hao kimesikika na serikali imeamua kutatua tatizo hilo.

"Katika kata yetu ya Themi, kumekuwapo na tatizo kubwa la muda mrefu kwa wanawake kukosa huduma ya kujifungua, kiasi kwamba inawalazimu kuhama makazi ili kusogea karibu na huduma.

...Ila kwa sasa, tunaishukuru serikali, kwa kulitambua hilo na kutoa fedha kupitia Jiji letu, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto, ambalo litalokuwa na wodi ya wazazi na chumba cha upasuaji."

Alisema kuwa mchakato wa ujenzi wa jengo hilo, wameuanza miaka mitatu iliyopita na wanashukuru kupata ushirikiano wa serikali, kwa sababu ya changamoto za kujifungua, zilikuwa ni kubwa kutokana na umbali wa kufuata huduma hiyo.

Alisema katika kikao walichokaa wamekubaliana siku za usoni kuanza mchakato wa ujenzi huo ikiwemo kutangaza tenda na wamepanga ifikapo Machi mwaka huu, ujenzi wa jengo hilo uwe umeanza mara moja.

"Fedha hizo tayari zimeshaingia kwenye akaunti ya kituo na leo tumefanya kikao za maamuzi namna ya kutumia fedha hizo na tumekubaliana matumizi sahihi ya fedha za serikali na hatutachelewesha mradi huu na tutakuwa tukishirikiana na Jiji la Arusha ili kuharakisha mradio huo,"alisema.

Kinabo aliwaambia wananchi wa kata hiyo kuwa wavumilivu wakati mchakato wa ujenzi unafanyika na wanatarajia ifikapo katikati ya mwaka huu jengo hilo liwe limekamilika.

Aidha, mjumbe wa kamati hiyo, Catherine Nyabamba, aliishukuru serikali kwa kuwapatia fedha za ujenzi wa jengo hilo, kwani litaokoa maisha ya kinamama wanaojifungua ambao hapo awali walipata changamoto kubwa.

Alisema wananchi watanufaika na mradi wa jengo hilo, pindi litakapokamilika na kuwapunguzia gharama walizokuwa wakizitumia wakati wa kuwapeleka wake zao kupata huduma za kujifungua hasa nyakati za usiku.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Zaina Foundation, Zaina Njovu akitoa elimu kuhusu haki ya kidijitali kwa waandishi wa habari wanawake wa mkoani Kilimanjaro, wakati wa mafunzo yaliyofanyika mjini Moshi juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## UVCCM wahamasishana kugombea nafasi za uongozi

**Na Steven William,** MUHEZA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa umewataka wanachama wake kujitokeza kwa wingi kugombea uongozi ndani ya umoja huo katika maeneo yao.

Wito huo ulitolewa jana na Makamu Mwenyekiti wake, Rehema Omari, wakati akizungumza na wanachama wa UVCCM na wa CCM wilayani hapa Mkoa wa Tanga.

Ni baada ya kufungua tawi la vijana wa UVCCM Mlimani Park liliopo Mtaa wa Mdote Kata ya Majengo wilayani hapa.

Rehema alisema wanachama wa umoja huo wanatakiwa kutambua kuwa wana nafasi nyingi kugombea ndani ya umoja huo kwa ajili ya kuimarisha CCM.

Alisema kila mwanachama wa jumuiya ana haki ya kugombea nafasi hizo na wakati ukifika wachukue fomu na kujiandikisha katika daftari la kudumu la mpigakura.

"Na sisi tukiwa kama viongozi wenu tutahakikisha tunasimama imara kuhakikisha nafasi hizo vijana wanazipata," alisema Omari.

Aliongeza kuwa inatambulika kuwa hakuna kiongozi bora atakayepatikana kama hajapitia tanuri la UVCCM na kwamba jumuiya hiyo ndio inayoandaa vijana ambao ni taifa la kesho na wa siku zijazo.

Katika hatua nyingine; kiongozi huyo aliwaagiza Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dk. Jumaa Mhina kuhakikisha mikopo ya asilimia 10 ya halmashauri itakapotoka wapewe kipaumbele wanachama wa UVCCM wa shina hilo.

# Serikali yajenga shule ya wasichana kumaliza ndoa za utotoni

**Na Mary Mosha,** SIHA

WATOTO kike wa jamii ya kifugaji katika maeneo ya Wilaya ya Siha, Longido na maeneo jirani wataondokana na ndoa za utotoni baada ya serikali kujenga Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kilimanjaro ambayo inagharimu takribani Sh. bilioni tatu.

Shule hiyo ya mchepuo wa sayansi iliyopo Kijiji cha Mawasiliano Kata ya Gararagua yenye eneo lenye ukubwa wa ekari 50 imekamilika kwa asilimia 95.

Akizungumza jana mara baada ya kukagua mradi huo wa shule , Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu alisema tayari shule hiyo imekamilika kwa asilimia 95 na wamepokea wanafunzi wenye ufaulu wa alama A.

"Serikali imejenga shule hii ili kutokomeza mimba za utotoni, ukatili na wasichana kutofikia malengo yao, hivyo hakikisheni wote mnafika kidato cha nne kwa ufaulu wa alama ya kwanza, kwenda kidato cha sita na kwenda chuo kikuu ili kuleta matokeo chanya katika taifa letu, "alisema Babu.

Akisoma taarifa ya shule hiyo, Mkuu wa Shule, Mariana Msangi alisema hadi sasa wamepokea wanafunzi zaidi 140 wa kidato cha kwanza na cha pili.


"Tumepokea wanafunzi baada ya ujenzi kukamilika ambapo ilianza Septemba mwaka jana, tulijenga mabweni nane, madarasa 12, bwalo, maabara nne, jengo la utawala, nyumba za watumishi, jengo la wagonjwa, matundu 16 ya vyoo na kwa sasa tunaendelea na ujenzi mdogo huku wanafunzi wakiendelea kupata elimu ,"alisema

Aidha mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Dankan Urassa alisema licha ya shule hiyo kutarajiwa kuchukuwa wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ila bado itawasaidia watoto wa kike kufikia malengo yao.

"Ujenzi huo unakamilika ikiwa ni pamoja na kujenga ukuta utakaowasaidia wanafunzi kukaa salama zaidi katika eneo hilo pamoja na kuweka ulinzi wa eneo," alisema Urassa.

Baadhi ya wananchi wakizungumza na Nipashe akiwemo mkazi kutoka Kijiji cha Mawasiliano, Embakas Molell alisema wamehamasika kusomesha watoto wa kike baada ya baadhi yao kupata elimu kutoka kwa wanaharakati.

Alisema baada ya kuhitimu wameweza kuisaidia jamii katika masuala ya afya, elimu pamoja na kufanya ujenzi wa nyumbani kwao.





# 40 mbaroni wizi, ulanguzi wa sukari

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani hapa linawashikilia watu 40 kwa tuhuma mbalimbali za wizi, akiwamo mfanyabiashara kwa kulangua sukari kinyume na bei elekezi ya serikali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Janeth Magomi, alisema watuhumiwa hao walikamatwa kufuatia msako uliofanyika maeneo mbalimbali dhidi ya uhalifu kuanzia Januari 21 hadi Februari 27, mwaka huu.

Magomi, alisema katika msako huo pia walikamata mali zinazodhaniwa kuwa za wizi na vielelezo vyake zikiwamo nyaya za umeme za Mradi wa Nishati Vijijini (REA) wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

"Tumekamata nyaya za umeme rola mbili za mradi wa REA, TV 6, pikipiki tatu, solar moja, nondo sita, mashine ya kusukuma maji, viti 12, deki, meza mbili, fremu tano za meza, ngozi ya chatu," alisema.

Alitaja vitu vingine kuwa dawa za kulevya aina ya bangi gramu 2,190, kete 23 na misokoto 121, pombe haramu ya gongo lita 11 na mitambo miwili ya kutengenezea pombe hiyo.

Kamanda huyo, alisema kesi 10 walizipeleka mahakamani na watuhumiwa kufungwa jela.

Akizungumzia kuhusu ajali za barabarani, alisema wamekamata makosa 5,026 na kuwatoza faini ya papo kwa papo madereva huku watatu wakifungiwa leseni zao za udereva.

Kuhusu mfanyabiashara huyo, alisema wamemkamata kwa tuhuma za kumuuzia mwananchi mifuko nane ya sukari kinyume na bei elekezi ya serikali.

Hata hivyo hakuzungumzia kwa undani Zaidi kuhusiana na mfanyabiashara huyo na kusisitiza wanaendelea kuwasaka wengine wanaouza sukari kinyume na bei elekezi na kuonya wakibainika wataendelea kuchukuliwa hatua kali za kisheria.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (kushoto), akizungumza baada ya kusikiliza kero za wananchi katika eneo la Soko Kuu, Manispaa ya Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# DC aonya rushwa vitambulisho vya taifa

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Wilaya ya Tabora Mjini mkoani hapa, Louis Bura amewaonya viongozi wa serikali za mitaa na kata wa Manispaa ya Tabora kutojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa kwa wananchi wakati wa ugawaji wa vitambulisho vya Taifa.

Bura alitoa onyo hilo juzi wakati akizungumza na wajasiriamali katika Semina iliyoandaliwa na Benki ya CRDB Tawi la Tabora baada ya uzinduzi wa mtaji wezeshi kwa vijana na wanawake kupitia akaunti ya Imbeju.

Alisema Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imetekeleza agizo la serikali la kupeleka vitambulisho katikaofisi za serikali za mitaa na kata, hivyo wasitumie nafasi zao kwa kutaka vijisenti ambavyo vitaweza kuwaingiza kwenye matatizo. "Nawatahadharisha kwa atakayekiuka agizo la serikali hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake na mpaka sasa nimeliagiza Jeshi la Polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(TAKUKURU) kuwafuatilia kitakachotokea naomba tusilaumiane," alisisitiza Bura.

Aliwahimiza wananchi kwenda kuchukua vitambulisho vyao ambavyo ni muhimu sehemu yeyote watakayokwenda ili kuepuka usumbufu na kutotambulika kuwa sio raia wa Tanzania.

Kwa upande mwingine, aliwataka vijana na wanawake waliowezeshwa kupata mikopo kutoka CRDB kutumia fursa hiyo kuondokana na utegemezi katika kuajiriwa na kukuza mitaji yao.

# Wajawazito wajifungulia kwa sangoma

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAJAWAZITO katika Kata ya Bulige Halmashauri ya Msalala Mkoa wa Shinyanga wataondokana na adha ya kujifungua kwa waganga wa jadi maarufu kama sangoma baada ya ujenzi wa Kituo cha Afya Bulige kukamilika mwezi huu na kuanza kutoa matibabu.

Hayo yalisema juzi na Mhandishi wa Miundombinu wa Halmashauri hiyo, Magoto Juma wakati akitoa taarifa za ujenzi wa kituo hicho kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mganga Abdulfadhil wakati wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa ilani ya chama hicho katika kata hiyo.

Juma alisema hadi sasa wamekamilisha ujenzi wa majengo manne kati ya matano kwa gharama Sh. milioni 615 na kiasi kingine Sh. Milioni 45 kitatumika kwa ujenzi wa jengo ililosalia. Fedha hizo zimetolewa na Serikali.

Alisema halmashauri hiyo imetoa Sh. milioni 95 kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kukamilika ujenzi huoo

Vilevile, alisema serikali imetoa Sh.milioni 300 kwa ajili ya kununua vifaa tiba na kwamba vilivyofika kituoni hapo mpaka sasa vina thamani ya Sh. milioni 50 pekee.

Akizungumza baada ya kupokea taarifa hiyo, Abdulfadhil, alisema ujenzi wa kituo hicho ukikamilika, itakuwa suluhisho la kero kwa wakazi hao ikiwemo kutembea umbali usiopungua kilometa 10 kwenda Kata ya Ngaya kupata matibabu.

Aliwataka wakazi hao kuacha tabia ya kwenda kwa waganga wa jadi kujifungua kwa vile wanahatarisha maisha yao kwa sababu hawana utalaamu wa kitabibu.

Diwani wa Viti Maalumu wa Kata ya Ngaya, Lidyaa James, alisema kukamilika kwa kituo hicho kutasaidia kuondoa msongamano wa wagonjwa kwenye Kituo cha Afya Ngaya na kupunguza vifo vya wajawazito vitokanavyo na uzazi.

Awali baadhi ya wakazi hao, walisema ubovu wa barabara katika hiyo ni chanzo cha wajawazito kwenda kujifungulia kwa wagaga wa kienyeji na kuchangia vifo vyao na watoto kutokana na kukosa utalaamu wa kitabibu.

Kwa mujibu wa wakazi hao, kituo cha afya kipo kata jirani ya Ngaya kipo mbali na maeneo yao hali inayowalazimu wanaohitaji huduma za matibabu kutembea umbali mrefu na wajawazito kujifungulia njiani.

Mmoja wa wakazi hao, Pass Masonga, alisema licha ya kero ya barabara, kukosekana kwa kituo cha afya katika kata hiyo kwa kiasi kikubwa limechangia kukimbilia kwa waganga hao maarufu kama sangoma kupata tiba za jadi.

"Kwa hali hii tunashindwa kuwasafirisha wagonjwa kwenda vituo vya afya Ngaya, Segese na Chela kutokana na mitikisiko hasa wa usafiri wa pikipiki zinapopita kwenye mashimo, hali hii inawatia hofu wajawazito na kulazimika kwenda kwa waganga wa jadi karibu na maeneo wanaoishi kujifungua," alisema. Happynes Juma, alisema zahanati iliyopo inakabiliwa na wagonjwa na haina watoa huduma wa kutosha.

Happnes, alishauri majengo yaliyokamilika kwenye kuwa kituo cha afya kinachojengwa yaanze kutoa huduma za wagonjwa wa nje (OPD) ili kuondoa tatizo la wagonjwa kukimbilia kwa sangoma kupata tiba.



Ukurasa 12

**KIKUNDI VIJANA NA MKWANJA...**

NGO yakusanya vijana 239 na kuwasuka, wanatoka kibiashara, yumo mwenye ulemavu




Ukurasa 13


Usomaji huu wa magazeti redioni utazamwe upya


# BUFE

IJUMAA MACHI 1, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ukurasa 14

## Kikundi cha 'vijana wasiochagua kazi' wasimulia wanavyomea chini ya SIDO

# Rais alivyoliandaa Bwawa Nyerere kufuta shida umeme, ziada bidhaa mpya kimataifa

• Biteko: Mteja Zambia yu sokoni akisubiri megawati 70

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, mwaka juzi alishuhudia ujazaji maji Bwawa la Umeme la Julius Nyerere, akipongeza hatua zilizopigwa, licha ya changamoto na hujuma zilizoshuhudiwa wakati wa kuanzishwa kwa mradi huo.

Hiyo ilikuwa Machi 22, 2022 akisema mradi huo utasaidia kukabiliana na mafuriko ya kila mara Mto Rufiji, pia kuimarisha kilimo cha umwagiliaji.

"Nataka nitoe ahadi kwenu ndugu wa Tanzania kwamba nitausimamia mradi huu hadi ukamilike." akatamka Rais Dk. Samia Suluhu, katika matarajio ya kuzalisha megawati 2,115 za umeme kitaifa, wakati huo .

Rais akafafanua kuwa handaki la kuchepusha maji lina urefu wa mita 700, yaani sawa na viwanja saba vya mpira wa miguu lilijengwa miaka mitatu kabla kwa gharama yake takribani shilingi bilioni 235.

Sasa hatua ya kuzindua mitambo inayofua umeme, inatajwa kuihamisha nchi kutoka upungufu wa kati ya megawati 200 na 400 za umeme, hadi ziada ya megawati 70, pale mitambo yote itakapofanya kazi mwezi huu.

Bwawa hilo pia lina sifa ya pili, kuwa kivutio cha watalii kwa kuwa liko ndani ya hifadhi na litabadili kabisa taswira ya hifadhi hiyo na thamani yake kuongezeka ndani na nje ya Tanzania.

Hadi wakati huo mwaka juzi, mradi ulishafikia asilimia 78 ya utekelezaji wake tangu kuanza kujengwa, huku katika uzindu-zi, Rais Dk. Samia akaahidi kufutika kilio cha umeme kitaifa.

Maharage Chande, aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), akaweka wazi makadirio kuwa misimu miwili ya kipindi cha mvua, itaweza kujaza maji katika bwawa hilo.

"Tunaanza kujaza maji mwezi huu wa Desemba (2022) ambapo kuna mvua za vuli, pia tunategemea mvua za masika mwezi Machi 2023, ambazo zitakuwa mvua za msimu wa kwanza, pia tutapata vuli ndani ya kipindi hicho.

"Kisha tutapata zile za masika katika mwaka 2024 pamoja na vuli ya kipindi hicho, hivyo mvua mbili kubwa za masika zinaweza kujaza bwawa kwa hesabu zilizopo," akasisitiza Chande.



Sehemu ya mtambo wa kuzalisha umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. **PICHA: MTANDAO**

Sasa hatua ilikofika wastani wa wiki mbili hadi sasa, Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, akasema majaribio ya Mtambo Namba Tisa kwenye Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere wa Megawati 235 yamekamilika, hivyo kutatua changamoto ya mgao wa umeme nchini.

Wiki hii, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, anasema: "Kwa ratiba tulio nayo ya kawaida, umeme huu ulikuwa utufike mwezi wa sita (Juni, 2023), lakini kwa msukumo mkubwa wa Raisw Samia, leo tunafanikisha.

Wiki moja iliyopita, Naibu Waziri Mkuu Dk. Biteko, akatangaza uzinduzi wa mradi unatarajiwa kufanyika mwezi huu, Rais Dk. Samia akiwa na mgeni wake, Rais wa Misri Albdel Fatah Alsisi, kukiingizwa katika Gridi ya Taifa, jumla ya megawati za umeme 470.

**UMEME KUUZWA ZAMBIA**

Hadi sasa inatajwa soko la kuuzwa ziadfa ya umeme nchini Zambia, unaosafirishwa kwa njia maalum ya, ikipita Iringa hadi nchini Zambia (TAZA), mradi uliοazna mwanzo wa mwaka jana, kwa matarajio ya kwisha mwezi Januari mwaka ujao.

Njia hiyo inatajwa kusafirisha umeme kilovoti 400, pia utaimarisha upatikanaji umeme katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Rukwa.

Pia, akizungumza wiki hii na chombo kimoja cha kimataifa, Dk, Bitelo akasema itafunga fursa Tanzania kufanya biashara ya umeme katika nchi za Kusini mwa Afrika na ndani ya Afrika Mashariki.

Mnamo Julai mwaka 2022, aliyekuwa Waziri wa Nishati, January Makamba, akafafanua kuwa eneo ambako kungejengwa kituo cha kupoza na kukuza umeme cha Tunduma wilayani Momba, mkoani Songwe ni kati ya vituo vitano vya kupoza umeme vitakavyojengwa kwenye mradi huo.

Mratibu wa Mradi huo, Mhandisi Elias Makunga, anasemja utatekelezwa kwa gharama shilingi Trilioni 1.4 ambazo tayari Tanzania inazo na kwamba mradi utakuwa ni kiunganishi cha kwanza cha umeme wa juu kati ya Nchi Wanachama wa Kusini mwaka Afrika na Nchi Wanachama wa Mashariki mwa Afrika (EAPP).

Inatajwa kuwa ni hali itakayochagiza biashara ya umeme, ikiwezesha Tanzania inaweza kuuza umeme nje ya nchi pale inapokuwa na ziada, pia inamudu kununua umeme huo, pale itakapotokea upungufu.

Wakati mradi huo unaandaliwa, serikali ilishatenga shilingi bilioni 23.1 za kulipa fidia kwa wananchi zaidi ya 6,198 waliopisha mradi huo.

FEDHA

KIKUNDI VIJANA NA MKWANJA...

# NGO yakusanya vijana 239 na kuwasuka, sasa wanatoka kibiashara, yumo mwenye ulemavu

**Na Beatrice Philemon, aliyekuwa Mwanza**

UNAPOZURU Mwanza, jiji la pili kwa ukubwa nchini, kuna mradi unaoitwa 'Vijana na Mkwanja 'ulioanzishwa rasmi mwaka 2019 na Shirika lisilo la Kiserikali linaloitwa Mwanza Youth and Children Network (MYCN) katika wilaya ya Ilemela.

Lengo la kuwapo kwake ni kuwezesha vijana kujikwamua kiuchumi kupitia fursa zinazowazunguka, Meneja wa Mradi huo James James, akiiambia Nipashe wao ni shirika linalofanya kazi na vijana na watoto.

"Kupitia miradi hiyo waliweza kugundua kuwa kuna kundi kubwa la vijana lipo mtaani linashindwa kujikwamua kiuchumi, kwa sababu hawajui jinsi ya kufikia fursa zinazowazunguka ," anasema .

Pia, anataja vijana wengi wamefanya biashara ndogo kama vile utengenezaji sabuni, viungo vya chai, vikizalisha kwa kiwango cha chini na kushindwa kushindana sokoni, nyuma ya pazia wakiwa na elimu duni ya ujasiriamali na mitaji.

James anataja maeneo mengine ya kasoro ni sehemu zao za uzalishaji, pa kufanyia biashara ni duni na hawajui hali sahihi pa kupata masoko ya bidhaa wanazozalisha wahusika wakiboreshwa.

Baada ya wao wabunifu wa mradi kugundua changamoto hiyo, wakaamua kuanzisha mradi wa 'Vijana na Mkwanja' kwa ufadhili wa shirika la Foundation for Civil Society, ili kusaidia vijana kupata mafunzo na kujikwamua kiuchumi, kulingana na fursa tofauti zinazowazunguka.

James anaeleza: "Tulianza kwa kukusanya vijana kutoka kata ya Shibula, Nyamanoro, Ilemela, Nyasaka, Kitangire na Busweru na kutengeneza vikundi 13 vya vijana. Baada ya hapo, kila kikundi kilikuja na wazo lake, yaani wanataka kufanya nini na baadae tukaanza kutoa mafunzo."

### AINA YA MAFUNZO

Anasema, vijana walifundishwa elimu ya ujasiriamali, udhibiti fedha, uongozi, usimamizi na uendeshaji biashara, pia miradi.

Mafunzo yalitolewa na maofisa wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na MYCN kulingana na mahitaji yao.

"Tunashukuru shirika la Foundation for Civil Society kutupatia Dola za Kimarekani 55,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi, ambao umesaidia vijana kupata mafunzo ya aina mbalimbali" anasema.



Veronica Gideon (wa kwanza kushoto mwenye kilemba cheusi), akionyesha bidhaa alizotengeneza baada ya kupata mafunzo katika maadhimisho ya Wiki ya Vijana, yaliyofanyika mkoani Kagera, Kushoto ni Ofisa Maendeleo ya Vijana Wilaya ya Ilemela, Lucy Nicholous Matemba na kulia kwake, Lilian Boniphace, mnufaika mwenzake wa mradi wa vijana. **PICHA ZOTE: BERATRICE PHILEMON**

**"Nashukuru Mungu nimeweza kubadlili mtazamo wa watu hapa wilayani kwetu kuhusu watu wenye ulemavu**



Richard Kashinje, kijana mwenye ulemavu wa viungo akiwa ofisini kwake akitengeneza viatu.

### ZAO LA MRADI

James anafafanua kuwa, jumla ya vijana 239 wameshanufaika na mradi, hata wengi wamehama kutoka uzalishaji mdogo kwenda wa kati, biashara nyingi zimerasimishwa na zinashindana kwenye masoko makubwa, akitaja hasa bidhaa za ngozi, pochi, chakula, vinywaji (wine) na tui ya karanga (peanut butter0.

Anasema, vijana mitaji katika, huku zaidi ya shilingi milioni 30 kilitolewa kwa vijana na halmashauri, wakapatiwa maeneo ya biashara, sasa wananufaika na fursa za masoko kimkoa, baadhi ya bidhaa zikivuka mpaka wa nchi.

James anafafanua, wameanzisha kiwanda cha kutengeneza matofali, sasa kikapatiwa tenda za serikali kupeleka matofali ya ujenzi wa shule , pia hata watu binafsi, shirika la MYCN likiendelea kuwaunganisha na wadau wengine, kulingana na kazi wanazozifanya.

### FURSA ZA WILAYANI

Hapo James anataja fedha zinazotolewa na halmashauri husika kwa ajili ya vijana, maeneo yanayotolewa na serikali kwa vijana kufanyia biashara kupitia SIDO, vilevile mafunzo kwao wajasiriamali chipukizi.

Eneo lingine msimamizi James analofafanua, ni halmashauri yao inatengeneza miundombinu rafiki kwa ajili ya kazi zinazofanywa na vijana.

Anaendelea: "Kuna programu tofauti tofauti kwa ajili ya kusaidia vijana wajasiliamali, kwa mfano kulea vijana wajasiriamali wadogo mpaka wakue kupitia programu... vijana."

### MNUFAIKA WA MRADI

Veronica Nyamweko, kijana mama wa umri miaka 24 anayeishi katika kata ya Buswelu, wilayani Ilemela, mkoa wa Mwanza. Anatoka katika orodha ya vijana 239 walionufaika na mradi.

Veronica alifunzwa na SIDO kwa kushirikiana na shirika la MYCN), namna ya kusindikaji na utengenezaji bidhaa mbalimbali.

Eneo lingine analitaja kuwa utunzaji pesa, kuhudumia wateja na masoko, namna ya kupata mikopo serikali ya asilimia nne - vijana, jinsi ya kutangaza biashara kwa vipeperushi, ikiwamo kwenye maonyesho au mtu mmoja mmoja na kuwa na kadi ya biashara.

Mafaniko yake, anayafafanua kwamba:" Nimeweza kuanzisha biashara ya usindikaji wa viungo vya chakula kama vile tea masala, pilau masala, tangawizi ya unga, peanut butter, garlic paste, na garam masala.

"Nimeweza kusaidia familia yangu, kusomesha wadogo zangu watatu, kurasimisha biashara yangu kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na kupata GSI Bar-Code," anasema.

Pia, anajivuna kutangaza na kuuza bidhaa zake mtandaoni kwa kutumia mtandao, akipata wateja kwa njia ya anazotaja 'Instagramu na WhatsApp'.

Hivi sasa, Verionica anasema, amepata eneo maalumu la kufanyia biashara yake, kajenga nyumba ya kisasa, mtaji umeongezeka kutoka shilingi 40,000 hadi 400,000, hatau ambazo hakuwahi kuzifikia.

"Utumiaji wa vipeperushi na business card kwenye maonyesho mbalimbali na sehemu niliyopo zimenisaidia sana kupata wateja wapya, wateja wameongezeka kutoka asilimia 20 hadi 98. Ongezeko hili limetokana na bidhaa ya pilau, masala na 'tea masala' kuwa na soko zaidi," anasema.

Mjasiriamali Veronica, anasema awali kabla ya mafunzo alikuwa anabeba bidhaa zake kwenye pochi au begi na kwenda kuziuza mtaani.

Richard Kashinje, kijana mwenye ulemavu wa viungo (37) anayeishi katika kijiji cha Bukaga, wilaya ya Nyamagana, mkoa wa Mwanza ni miongoni mwa vijanao wamenufaika na mradi. Yeye amepata mafunzo kwenye bidhaa za ngozi, utengenezaji wa keki, viungo vya chai, pilau masala, utunzaji wa fedha na namna ya kukabiliana na changamoto kwenye biashara.

Kashinje na wenzake pia wamefundishwa namna ya kupata leseni za biashara 'Tin Number', jinsi ya kupata mkopo asilimia 10, mazingira ya afya na masuala ya demokrasia, kuangalia changamoto zinazowafanya vijana wasishindwe kazi za kujiajiri, baada ya kugundua elimu ya kujitegemea.

Anasema, alipata nafasi ya kushiriki wiki ya vijana ili kuona namna gani wafanyabiashara wenzake wanaboresha bidhaa zao.

Mafunzo yalitolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Manispaa ya Ilemela, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)

"Najivunia kulingana na elimu tofauti tofauti niliyopata kutoka kwa wataalamu mbalimbali nimeweza kujiamini kuwa kumbe kuwa mlemavu siyo kuishindwa kimaisha, sasa hivi nimefungua kampuni yangu inaitwa 'Kishili Supply'.

"Nimejiajiri mwenyewe, natengeneza viatu vya ngozi vya aina mbalimbali, mikanda ya ngozi, (pochi) 'wallet' kwa wanafunzi , wafanyabiashara na nimefanikiwa kuajiri vijana 15," anasema.

Kama alivyo mtangulizi wake, anajivuna amefanikiwa kujenga nyumba ya kisasa kupitia biashara ya viatu, huku awawasomesha wadogo zake, na amepata 'TIN number' kutoka TRA. Kashinje anafafanua kuwa, amesharasimisha biashara yake, kipato chake kimeongezeka kutoka shilingi milioni moja hadi milioni tatu kwa mwaka, anapata tenda kutoka kwa wateja mbalimbali ndani na nje ya mkoa wa Mwanza.

Kutanua ujuzi, anasema ameshawafundisha vijana 20 jinsi ya kutengeneza viatu na wao wameanza kutengeneza bidhaa za Ngozi. Pia, baada ya kushiriki maonyesho mbalimbali katika mkoa wa Mwanza na mingine, hivi sasa hivi jamii hamchukulii 'kama mlemavu', bali ni mtu 'kama watu wengine.'

Anasema ametumia fursa hiyo kuonyesha wenye ulemavu pia wanaweza kufanya kazi na kujiongezea kipato pasipo kuomba mitaani.

"Nashukuru Mungu nimeweza kubadlili mtazamo wa watu hapa wilayani kwetu kuhusu watu wenye ulemavu," anasema.

Anajigamba, hivi sasa ana ujasiri wa kufanya biashara na biashara yake inatambulika, fedha anazopata anatumia kununua malighafi,analipa mshahara kwa wafanyakazi, anasaidia familia yake, wazazi na shughuli nyingine.

"Nashukuru MYCN kuniwezesha kupata elimu hii na kushiriki kwenye maonyesho ya biashara katika mkoa w Kagera, Mwanza City Mall, East Africa ambayo yamesaidia biashara yangu kujulikana na kupata tenda zaidi," anasema.

Wito wake, nawaomba wadau mbalimbali wamsaidie kujenga jengo la viwanda vya kutengeneza bidhaa na pia kumnunulia mashine zinaoitwa ' skiving machine, post bed stitching machine, cylinder bed machine' na 'flatbed stitching machine' kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za ngozi.

### MKURUGENZI MYCN

Mkurugenzi Mtendaji wa MYCN, Brightius Titus alishukuru shirika Foundation for Civil Society kuwapatia fedha za kusaidia vijana kupata mafunzo na hatimaye kuanzisha miradi mbalimbali ya kujikwamua kiuchumi .

Anasifu vijana wamefanilkiwa kutengeneza sabuni bidhaa kama; spices, wine, batiki, dagaa za kukausha kwa kutumia moshi, kutengeneza , peanut butter, viungo vya pilau, unga lishe, biashara ya utengenezaji wa tofali, wengine wananunua avocado na kusambaza mijini na wamefanikiwa pia kununua mashine ya kutotolesha vifaranga.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Usomaji huu wa magazeti redioni utazamwe upya






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

HIVI karibuni chombo cha habari kilimkariri Meneja wa Huduma za Utangazaji wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Andrew Kisaka akisema kwamba mamlaka hiyo itawachukulia hatua watangazaji wanaosoma magazeti kwa mbwembwe, na kuongeza vitu visivyotakiwa kwenye matangazo yao.

Hata hivyo baada ya habari hiyo kusambaa, muda mfupi baadaye, chombo kingine kikaikariri TCRA kikisema alikaririwa vibaya, kwa kuwa hakuna kanuni inayokataza magazeti kusomwa kwa mbwembwe.

Kituo kingine cha redio kikashangilia kauli hii ya pili ya kutokuwapo kanuni ya kuzuia kusomwa magazeti kwa mbwembwe, huku watangazaji wa kituo hicho wakihanikiza kuwa kinachofanyika ni usasa, tofauti na ilivyokuwa kwenye ukale.

Kwa maana hii, ni kuwa usomaji wa mbwembwe unaendana na kizazi kipya huku wanaosoma kwa utulivu, wakiendelea kung'ang'ania ukale usio na mvuto kwa wasikilizaji wanaohitaji kuchangamshwa.

Ni kweli kuwa kila kituo cha habari kina sera yake ya utangazaji au uandishi wa habari, ingawa maadili ni yale yale yasiyokiuka utendaji kazi na uendeshaji wa vyombo katika dhima yao ya kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha.

Hivyo basi kama kuna watangazaji wanataka kutangaza huku wakicheza ngoma au wakiimba huo ni utaratibu wao, ili mradi wanajua ujumbe wanaoutaka unaifikia hadhira, bila kukiuka maadili ya utangazaji.

Pengine ndiyo sababu siku hizi vituo baadhi vya redio na luninga, vinaajiri wasanii hata kama hawana taaluma ya tasnia ya habari, kwa sababu tu wanakubalika katika jamii na ndiyo sababu hata nidhamu katika vituo hivyo imeshuka.

Ila wanapaswa tu kujua kuwa, kizuri chajiuza kibaya chajitembeza, kwamba kisipojiangalia, kinaweza ama kujikuta kina wasikilizaji wengi au wachache, kutokana na kwamba uzuri wa kusikia na kusikiliza umo masikioni mwa msikilizaji.

Kinachosikitisha na pengine kugusa wamiliki wa magazeti yanayosomwa kwenye vyombo vya kielektroniki kwa maana ya redio na luninga, ni hicho kingine ambacho pia kilisemwa na TCRA, cha kusoma vichwa vya habari na kuingia kwa kirefu kwenye stori.

Ingawa watangazaji niliowasikia kwenye kituo hicho cha redio walitamba kuwa hilo halina tatizo, ni dhahiri kuwa hawaelewi ni nini athari kwa wenye magazeti kimauzo, ingawa naamini wanajua kuwa mauzo ndiyo injini ya kampuni za magazeti.

Endapo watangazaji hao wataendelea kuachwa watangaze habari kwenye magazeti kwa kusoma stori yote badala ya kichwa tu, maana yake ni kuwa msomaji akishasikia stori yote anakuwa hana haja ya kupoteza Sh 1,000 au Sh 2,000 zake kununua gazeti.

Kiini cha kuanzisha vipindi vya kusoma vichwa vya magazeti, ilikuwa ni kuwezesha wasomaji kujua yana nini na kuamua kuyanunua au kuacha kulingana na atakipata baada ya kusikia vichwa vya habari.

Ni bahati mbaya, kwamba baadhi ya vituo vya redio na luninga, badala ya kufanya hivyo, na pengine kwa kukosa maudhui ya kutangaza kwenye vipindi vyao, huamua kusoma kila kitu kwenye gazeti ili kufidia upungufu unaowakabili. Ikumbukwe, mwaka 2017 akiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alitoa tamko likizuia vituo hivyo kusoma habari yote na badala yake viishie kwenye vichwa tu.

Inakumbukwa, kuwa vituo vilivyokuwapo vilitii tamko hilo, na vinaendelea kufanya hivyo, tofauti na vilivyozaliwa baada ya tamko hilo na ndivyo vinasumbua kwa kushindwa kusoma vichwa tu na kujikuta vikifidia muda kwenye matangazo yao.

Ni dhahiri kuna baadhi ya watu hutaka kusikiliza kipindi cha magazeti kwenye vituo vya utangazaji, hivyo kipindi hicho kuwa kivutio cha wasikilizaji, halikadhalika vipindi hivyo husaidia mgazeti kuuza.

Kama hivyo ndivyo na ndivyo ilivyo, hapana haja ya redio na luninga kusoma habari yote, kwani vinaumiza magazeti kimauzo na hatimaye kifaida, na kama walivyotamba watangazaji hao, kuwa asiyetaka gazeti lake lisomwe aseme na wataacha, hiyo si sawa.

Kukosa kusoma magazeti asubuhi ni kukosa wasikilizaji, pia ni kukosa wanunuzi, hivyo jambo la msingi ni kuacha jeuri na kiburi na badala yake, kufikiria kuwa kusoma habari yote ni kuumiza wenye magazeti na hivyo ni vizuri kuachana na tabia hiyo.

Ni vizuri wenye vyombo vya kielektroniki kuwa wabunifu wa vipindi vipya zaidi badala ya kutumia habari zilizofanyiwa kazi na wengine, ambao ni waandishi wa habari magazetini, kufanyia vipindi.

Ifahamike kuwa, waandishi wa habari wanatumia nguvu na akili kutafuta habari, zinachakatwa na hatimaye kutolewa magazetini kwa faida ya kampuni husika, hivyo kituo kingine kinapochukua habari hizo na kuzitumia kama kipindi chake badala ya kugusia tu, haijakaa sawa.

BIASHARA

# Kikundi cha 'vijana wasiochagua kazi' wasimulia wanavyomea chini ya SIDO

## • Imewapangisha, inawatafutia soko...

**Na Christina Haule, Morogoro**

NI darasa la aina yake, vijana wamekalishwa chini, wakipewa somo kuachana na kuendekeza kukaa mtaani.

Inatajwa, katika mustakabali wa 'hapa kazi tu' na kazi iendeelee' daima nafasi ya kuchagua kazi izidi kutupwa, sasa watu wafanye kazi zinazohusisha mikono yao, ili kupata kipato na kubadilisha hali zao za maisha.

Kiongozi wa Kikundi cha Watu 10 wanaozalisha vifaa vya vyuma na uchakataji mazao ya kilimo, kiongozi wao, Aron Mnega, katika mzungumzo na Nipashe kwenye Mtaa wa viwanda wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) mjini Morogoro, anasema: "Unaposema kwamba ajira hakuna na kukaa mtaani tu hakutasaidia.

"Vijana wengi ukiwakuta mtaani wana tabia ya kuchagua kazi za kufanya, lakini uhalisia hakuna kitu kitakufanya uishi vizuri kama sio kutumia mikono yako.

"Maana ukifuatilia asilimia kubwa ya vijana wengi wamesoma na hawana ajira na wengine hawajasoma hawana ajira, lakini wanaishi wakiwa na ndoto za kuajiriwa kwenye viwanda vikubwa bila mafanikio. La muhimu ni kupambana na kujikwamua kiuchumi" anasema.

Hivyo Mnega anawataka vijana kutambua kuwa wakati ndio huu wa kubadilika na kujiunga kwenye mtaa wa viwanda SIDO unaowasaidia vijana kujiinua kiuchumi.

Mnega anasema, wao kwa kutumia mashine rahisi, hutumia uwezo wao kutengeneza vifaa aina mbalimbali kurahisisha mahitaji kwa jamii. wAnataja wanatengeneza madirisha ya vyuma, milango na mageti makubwa, huku akitaja vingine wanavyotengenzea ni mashine za kukaanga karanga, kukoboa na kusaga mahindi.


Pia, zimo za kuchakata mpunga uliovunwa, kupukucha mahindi, kukuna nazi, kukamua mafuta ya parachichi na kubangua karanga huku

Mnega ananapataja kimasoko, mahali hapo Mtaa wa SIDO, ni sehemu nzuri ya kutafuta wateja, pia panabaki kuwa soko zuri la bidhaa zao, kwa sababu SIDO ina utaratibu mzuri wa kuwatafutia wapangaji wao soko la bidhaa.

Aidha, anaishukuru SIDO kuwajengea majengo yanayowaleta mahali sahihi kibiashara ambako mitaani walikokuwa zamani kuna wakati walinyeshewa hata na mvua, lakini kwa sasa uzalishaji wao unafanyika katika mahali rafiki.

Lingine anataja tatizo la kukatika umeme ila mara lilikuwa likiwaathiri muda mrefu. Hata hivyo, siku chache ziliopita kuanza kufunguiliwa maji katika Bwawa la Nyerere kumeongeza umeme kitaifa.

Pia, Naibu Waziri Mkuu na Waziri Nishati, Dotto Biteko, ameahidi mwezi huu tatizi hilo liakoma kitaifa, baada ya kufunguliwa lango liginme la maji.



Kiongozi wa kikundi cha watu 10 wazalishaji wa vifaa vya chuma na uchakataji mazao ya kilimo, Aron Mnega, akionyesha mashine wanazotengeneza ya kukaanga karanga.



Mmiki wa kiwanda kidogo cha kuchonga vyuma, Dedu Ng'imba, akionyesha mashine wanazotumia kutengeneza vipuri vya mashine za viwandani. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**

### WADAU WAANIKA MZIZI

Mmoja wa vijana kutoka eneo la Kihonda mjini hapa, Vincent Jackson, anasema changamoto ya ukosefu wa ajira, ni janga kubwa kwa vijana nchini, sambamba na suala la kukosekana mitaji wa kuwezesha biashara zao, hata za kutumia mikono yao.

Mmiliki wa kiwanda kidogo cha kuchonga vyuma Dedu Fabrication Work, Dedu Ng'imba, akiwa katika mtaa wa Viwanda SIDO Mkoa wa Morogoro, anashauri shirika hilo kuwakusanya wenye viwanda vidogo wajumuike kikazi, ndio zao lake ufanisi kikazi.

Anafafanua kwamba ni jambo litakalowasadia kupata wateja kwa wepesi, wakainuka kimtaji huku wakikuza uchumi wao kwa pamoja.

Ng'imba anasema, ujenzi wa majengo hayo utasaidia wenye viwanda kuwa na muunganiko mzuri kikazi, hivyo wateja wanaohitaji huduma mbalimbali wanaipata katika eneo moja.

Anatrumia mfano wao, wanashughulika na uchongaji vipuri na spea za viwandani, kuchonga vipuri vya kilimo, kutengeneza mashine mbalimbali za kusaga, kukoboa na kupukuchua mahindi sambamba na kushauri wateja kuhusiana na mashine za kilimo.

Anasema kwa sasa wanauza bidhaa zao katika viwanda mbalimbali vinavyochakata mazao, vinavyotengeneza nguo, pia magunia na kwa wakulima mbalimbali.

Ng'imba anasema, wanaofanya biashara katika Mtaa wa Viwanda SIDO, hutoa punguzo kwa wateja, hasa wanaoenda kununua bidhaa zao tofauti na walivyokuwa nje ya eneo hilo.

> **Ujenzi wa majengo hayo utasaidia wenye viwanda kuwa na muunganiko mzuri kikazi, hivyo wateja wanaohitaji huduma mbalimbali wanaipata katika eneo moja.**

### CHANGAMOTO ZILIZOKO

Mzalishaji Ng'imba, anasema wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji mdogo wa vifaa, hivyo anaiomba serikali kuhakikisha inadhibiti tatizo la kukatika kwa umeme, linalorudisha nyuma maendeleo ya viwanda nchini.

Aidha anawashauri wenye viwanda vidogo waliopo nje ya mtaa wa viwanda SIDO, kupeleka maombi yao SIDO, ili kuongeza hali ya kuongeza majengo mapya na kukabiliana na changamoto ya uchache wa majengo kwenye mtaa huo, kwa sababu majengo ya SIDO ni mapana na ya nafasi tofauti na walivyokuwa nje ya hapo.

### KUTOKA SIDO

Meneja wa SIDO mkoa wa Morogoro Joan Nangawe, anasema majengo ya mtaa wa viwanda yalianza kujengwa mwaka 2020 na kukamilika mwaka 2021, yakiwa na lengo la kuwakusanya wazalishaji wadogo na kufanikisha kuwainua kibiashara na hatimaye kukua kiuchumi.

Meneja Nangawe anasema majengo hayo yamegharimu jumla ya shilingi Milioni 400 zilizotokana na fedha za maendeleo za Serikali.

Anasema mpaka sasa kwenye mtaa huo wa viwanda SIDO kuna jumla ya wapangaji sita ambao wanazalisha bidhaa za aina tofauti tofauti.

Nangawe anasema, mpango wa serikali ni kuendeleza mtaa wa viwanda kwa kuendelea kujenga majengo mengine na kwamba SIDO inaendelea kuandika maombi kupitia bajeti zake mbalimbali, ili kupata fedha za maendeleo na kujenga mengine yatakayokidhi mahita ya waombaji.

"Wapo waombaji wengi ambao hutaka kupanga katika mtaa huo, hivyo kukosa nafasi kutokana na majengo yaliyopo kuwa tayari yameshapata wapangaji na hivyo anawaomba kungojea awamu nyingine ya ujenzi itakapotokea" anasema.

Nangawe anasema, kwa sasa SIDO inaendelea kutekeleza majukumu yake makuu, ikiwamo kutoa mafunzo ya kuwawezesha wajasiriamali kupata masoko na kupata mikopo ya mitaji.

Nangawe anasema, SIDO hupokea watu wenye mitaji na hata wasio na mitaji na kuwapatia mikopo wawapo kwenye vikundi jambo linalosaidia kuinua kipato kwa vijana huku wengine wakipatiwa mafunzo ya kutengeneza bidhaa mbalimbali kwa lengo la kujipanua kiuchumi.





Mfanyabiashara wa vichwa vya ng'ombe, Yasin Joseph akiviandaa kwa ajili ya wateja wake, katika machinjio ya Mtaa wa Mbuyuni, Kata ya Kizota, jijini la Dodoma jana. Wanunuzi wa vichwa hivyo, huvitumia kwa kutengenezea supu.
**PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mfanyabiashara madini tanzanite afungwa jela miaka 15 kwa kuua

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dodoma imemhukumu kifungo cha miaka 15 jela mfanyabiashara wa madini ya tanzanite, Chacha Meng'anyi (43) kwa kosa la kuua bila kukusudia alilolifanya katika baa ya Platinums Park iliyopo jijini Dodoma.

Chacha alimuua mkazi wa Area C na mfanyabiashara jijini hapa, Devotha Ochido (41) kwa kumpiga risasi Aprili 23, 2022 majira ya saa 9:00 usiku katika baa hiyo.

Akisoma hukumu hiyo, Februari 26, mwaka huu, Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma, Suleiman Hassan, alisema maamuzi hayo yamezingatia mambo mbalimbali ikiwamo kosa hilo ni la kwanza kwa mtuhumiwa.

"Uamuzi huu umezingatia mambo mbalimbali ikiwemo mtuhumiwa kuwa hili ndilo kosa lake la kwanza kutenda lakini pia baada ya kufanya tukio hili alijisalimisha kwa vyombo vya sheria hii inaonyesha ni kwa namna gani alijutia kutenda kosa lile.

"Lakini pia kitendo cha mtuhumiwa kujisalimisha kwenye vyombo vya sheria na kukiri kosa kimesaidia kupunguza muda na gharama za kufanya uchunguzi pia mtuhumiwa tayari ameshakaa mahabusu kwa muda mrefu, hivyo kipindi hicho alichokaa mahabusu kimempatia fundisho"alisema Jaji Hassan.

Aidha, alisema pamoja na mshtakiwa kutoa utetezi lakini kosa alilotenda limesababisha marehemu kuacha watoto watatu ambao hivi sasa wanapata shida kutokana na kuondokewa na mama yao mzazi.

"Lakini pia mtuhumiwa alimpiga risasi marehemu kwenye maeneo hatarishi maeneo ya tumbo lakini pia kujeruhi watu ambao waliokuwa wakijaribu kuzuia tukio hilo lisitendeke, mshitakiwa alizuliwa na mlinzi wa baa lakini alikataa na kuamua kutumia silaha hiyo.

"Mshtakiwa alidiriki kusema mimi sidhulumiwi nitaua mtu. Kwa maoni yangu ukitizama hili ni miongoni mwa makosa ya kifungo cha maisha kimsingi kitendo ambacho amefanya mtuhumiwa ni kitendo cha kutisha kikemewe kwa sauti zote."

Alisema: "Lakini kwa kuwa mshtakiwa ni kosa lake la kwanza na bado ana umri mdogo mahakama inamuhumu kifungo cha miaka 15 na inatoa amri ya kutaifisha silaha yake aina ya pistol na kufutiwa leseni ya umiliki wa silaha hiyo".

Awali akitoa maelezo ya kosa la mauaji ya bila kukusudia kama yalivyosomwa mahakamani hapo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Lina Magoma, alieleza Mahakama kuwa Aprili 20, 2022 Chacha alifika jijini Dodoma akitokea mkoani Arusha kwa shughuli zake za kibiashara na kufikia kwenye nyumba ya wageni iitwayo Cheto Lodge maeneo ya Airport jirani na baa hiyo.

"Mshtakiwa aliendelea kuishi hapo hadi Aprili 22, 2022 ambapo majira ya saa 3 usiku alitoka kwenda kupata chakula na vinywaji kwenye baa hiyo, akiwa hapo alikutana na watu mbalimbali na kuwa na maongezi nao akiwemo marehemu."

"Mtuhumiwa aliendelea kuwepo kwenye baa hiyo huku akiwa na silaha yake ndogo aina ya pistol aliyoificha kiunoni hadi majira ya saa 9:00 usiku ambapo aliishiwa pesa za matumizi na ndipo alimuomba marehemu amuelekeze sehemu ya kutolea pesa yaani wakala."

"Ndipo marehemu akampeleka kwenye kaunta nyingine ya vinywaji vya kawaida iliyopo kwenye baa hiyo na kumkuta mhudumu aitwaye Babuu Issa ambapo alitoa Sh.200,000 kwa njia ya simu lakini ujumbe wa kuthibitisha kutoa pesa hizo haukurudi, hivyo mtuhumiwa alirudi alipokuwa amekaa,"

"Baada ya muda mfupi mtuhumiwa alipokea ujumbe mfupi kupitia simu yake unaothibitisha kutoa pesa ndipo akarudi tena kaunta kwa mtoa huduma Babuu na kumuonyesha ujumbe ule lakini Babuu hakutaka kumpa pesa hizo." alisema

Alisema kufuatia jibu hilo, mtuhumiwa alianza kufoka na kugonga meza ya kaunta huku akisema haiwezekani pesa yake ipotee kirahisi na akatoka nje na kisha kurudi tena ndani huku akiwa ameshika silaha ndogo aina ya pistol, mlinzi wa baa hiyo Hassan Idd akimsihii asifanye jambo lolote kwani pesa yake atapewa.

Alisema mtuhumiwa hakuonyesha kusikiliza wala kujali na badala yake akaelekea sehemu waliyokua wamekaa marehemu na marafiki zake na kisha kuanza kufyatua risasi ambazo zilimpata marehemu.

Mmliki wa baa hiyo, Haji Kweji alimfuata kujaribu kumzuia kufanya hivyo lakini alifyatua risasi zilizomjeruhi kwenye paja lake la kushoto.

Alisema mtuhumiwa pia aliendelea kufyatua risasi ambazo ziliwajeruhi watu mbalimbali na baadaye kujisalimisha kituo cha polisi

# RC atoa maagizo TARURA ujenzi, ukarabati barabara

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameitaka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) mkoani hapa kuwasimamia kwa karibu makandarasi wanaopewa zabuni za ujenzi na matengenezo ya barabara.

Amesema baadhi yao wamekuwa na miradi mingi na kusababisha miradi mingine utekelezaji wake kusuasua.

Serukamba alitoa agizo hilo jana baada ya kutembelea mradi wa ujenzi wa barabara inayoziunganisha kata tisa za Wilaya ya Manyoni unaogharimu Sh.milioni 900 na kutoridhishwa na kasi ya ujenzi ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 35 tu na unatakiwa kukamilika Machi 18 mwaka huu.

"Barabara hii inakwenda kuziunganisha kata tisa hivyo unaweza kuona idadi ya watu wanaotamani barabara hii iishe, mtu ambaye amefikisha asilimia 35 halafu tunajadili muda wa kumuongezea hapana, hapa lipo tatizo, kwa hiyo niombe Meneja TARURA Manyoni msimamieni huyu mkandarasi," alisema.

Serukamba alisema mkandarasi huyo aandikiwe barua kumjulisha kuwa TARURA haipo tayari kumuongezea muda baada ya mkataba wake kumalizika Machi 18, mwaka huu maana kumweleza kuwa ataongezewa muda hatafanya kazi kwa bidii.

Alisema: "Meneja wa Mkoa katika hili simamia Sh.milioni 900 ni pesa nyingi sana kwenye mradi huu kwasababu wananchi wanaisuburi hii barabara ambayo ni muhimu kuunganisha kata tisa, kaa na watu wako muone kama je tatizo ni majaluba, vifaa, fedha au hajaupa kipaumbele mradi huu," alisema.

Serukamba alisema tatizo baadhi ya wakandarasi wanakuwa na miradi mingi sana kwa hiyo kinachotokea anatoa kipaumbele kwa baadhi ya miradi kwa hiyo kama hasimamiwi kwa karibu mradi unachelewa kukamilika kwasababu anakuwa na miradi aliyoiwekea kipaumbele.

Aidha, aliwaagiza kuhakikisha wanalinda viwango vya maeneo ambako yanatakiwa kuwekwa changarawe kilometa 19 yaweke, sehemu za makaravati pia wafanya hivyo na maeneo ambayo ni ya mjini kuwekwe misingi ili barabara isiweze kuharibika.

Naye, Meneja wa TARURA Mkoa wa Singida, Mhandisi Ibrahimu Kibasa, alisema kusuasua kwa mkandarasi huyo kunatokana na mvua zinazoendelea kunyesha na kwamba ushauri uliotolewa watafanyia kazi.





## Iwungilo wajengewa kituo cha afya

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

ZAIDI ya wakazi 300,000 wa Kata ya Iwungilo Halmashauri ya Mji wa Njombe mkoani hapa wanatarajiwa kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu baada ya serikali kuanza mchakato wa kuwajengea kituo cha afya.

Akizungumza na Nipashe, Benjamini Mkulu aliiomba serikali kukamilisha ujenzi wa kituo hicho ili kuondokana na adha hiyo ya kutembelea umbali wa Zaidi ya kilomita 15 hadi kata nyingine kufuata huduma za afya.

"Hususani wamama wanaopata shida ya uzazi wanasafiri umbali mrefu hivyo tunaomba kikamilike haraka ili kitusaidie," alisema Mkulu.

Keneth Luambati, alisema hali ya huduma za afya katika kata hiyo zilikuwa ni hafifu kwa sababu walikuwa wanatumia zahanati ya kijiji.

"Kwa sasa wangetusaidia kwa yale majengo ambayo yapo tayari yangeanza kutumika, na hivyo tungepunguziwa kwenda hospitali ya Ikonda (wilayani Makete)," alisema Luambati.

Mariam Kaduma, alisema anaishukuru serikali kwa kuwajengea kituo cha afya na kuwaondolea adha waliyokuwa wakipata.

"Unaweza ukapima kliniki kule kati lakini kujifungulia unashangaa hospitali ya Kibena, tunashukuru kwa kutusogezea kituo hapa itatupunguzia vitu vingi hasa gharama," alisema Kaduma.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Iwungilo, Dk. Flavian Ntengo, alisema wakazi hao watanufaika na kituo hicho hasa wajawazito na watoto.

"Kwa maana huduma zitakuwa zimerahisishwa kwa mfano vijiji vya jirani ambavyo vina zahanati watakuwa na uwezo wa kuwapa rufaa wagonjwa wao hapa ambao wanamatatizo ambayo yameshindikana katika zahanati," alisema Ntengo.

Mtendaji wa Kata ya Iwungilo, Bonasius Mwalongo, alisema serikali imejenga kituo hicho ili wananchi waweze kunufaika na huduma za afya jirani na makazi yao.

"Tuna jengo la mama na mtoto, tuna jengo la upasuaji na tuna jengo la kufulia nguo ambapo wananchi wanachangia mchango wa shilingi 5,000 kwa ajili ya kuleta vifaa, mawe, mchanga na matofali, " alisema Mwalongo.

Alitoa wito kwa wananchi wa kuhakikisha wanaendelea kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa kituo hicho ili kikamilike kwa wakati na kuanza kutoa huduma.

# Wataalamu waagizwa kutokomeza kichocho, minyoo

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WATAALAMU wa afya wilayani hapa Mkoa wa Mbeya wameagizwa kutoa elimu kwa wananchi ya kujikinga na kutokomeza magonjwa yasiyopewa kipaumbele ikiwemo kichocho na minyoo ya tumbo hasa kwa watoto chini ya miaka 15 .

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Josephine Manase kwenye kikao cha Kamati ya Afya ya Msingi ya wilaya kilichofanyika juzi kilichowashirikisha wataalamu hao na wadau wa afya. Manase, aliwataka wataalamu hao kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kujenga vyoo ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko kikiwemo kipindupindu.

Aliwataka kuhamasisha wananchi kuwa na utaratibu wa kupima afya mara kwa mara ili kupunguza athari zitokanazo na magonjwa hayo yasiyopewa kipaumbele huku akiwasisitiza wananchi kuepuka imani potofu dhidi ya magonjwa hayo ambazo hupelekea madhara katika jamii ikiwemo kifo.

"Wapo watu wanaamini mtoto akikojoa damu ni ishara kuwa amebalehe na wengine amelogwa badala ya kumpeleka kituo cha afya wanampeleka kwa mganga wa kienyeji hii sio sawa ukiona dalili hizo mpeleke mtoto wako kituo cha afya akapate tiba sahihi," alisema Josephine.

Kwa upande mwingine, aliwaomba viongozi wa dini kuisaidia Serikali kutoa elimu kwa waumini wao dhidi ya magonjwa hayo yasiyopewa kipaumbele na kuchukua tahadhari.

Aliwataka wakazi wa wilaya hiyo kuacha imani potofu kuhusu chanjo na kinga zinazotolewa kwa watoto wao kwani Serikali imetumia gharama kubwa kuhakikisha inatokomeza magonjwa hayo ili waishi vizuri na kutengeneza kizazi chenye afya njema na akili timamu.

Hata hivyo, alisema wilaya hiyo imeweka mikakati ya kutokomeza magonjwa ya kichocho na minyoo ya tumbo kwa kuzingatia njia zote za kujikinga nayo.



Baadhi ya vijana wakipakia madawati kwenye gari, yaliyotengenezwa na mafundi jamii kwa ajili ya shule mbalimbali za msingi na sekondari za Jiji la Mbeya jana. Jiji hilo, limepanga kutengeneza zaidi ya madawati 6000, ili kumaliza tatizo la upungufu wa samani hizo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Makongorosi wapatiwa vifaa tiba

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKAZI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi wameondokana na tatizo la kutembea umbali mrefu kwenda kupata matibabu Hospitali ya Wilaya ya Chunya baada ya serikali kupeleka vifaa tiba kwenye Kituo cha Afya cha Makongolosi.

Wakazi hao walikuwa wakisafiri umbali wa zaidi ya kilomita 39 kwenda kupata huduma za upasuaji katika hospitali ya wilaya kutokana na kituo hicho kipya kukosa vifaa hivyo.

Wakizungumza wakati wa kupokea vifaa hivyo kutoka Bohari ya Dawa (MSD) juzi wakazi hao , walisema walianza kujenga kituo hicho kwa nguvu zao ili kuondokana na adha hiyo ya kukosa matibabu. Hilda Fande, alisema katika kituo hicho walikuwa wanapata huduma za kawaida za matibabu, isipokuwa za kufanyiwa upasuaji kutokana na kukosekana kwa vifaa.

Hilda, alisema huduma za kujifungua wajawazito, zilikuwa zinapatikana kwenye kituo hicho, lakini upasuaji wahudumu walikuwa wanaandikiwa rufani kwenda hospitali ya wilaya.

"Tunaishukuru serikali kwa kutusogezea huduma hizi hapa, kumsafirisha mjamzito kutoka hapa mpaka Chunya mjini ni gharama kubwa, hapa sasa tutajifungua hata kama kwa upasuaji," alisema Hilda.

Amos Mwazembe, alisema kituo hicho hakikuwa na majokofu ya kuhifadhia maiti hali iliyokuwa inawalazimu kwenda kuhifadhi miili ya ndugu zao katika hospitali hiyo ya wilaya.

Mwazembe, alisema kitendo hicho kilikuwa kinawaongezea gharama na kwamba baada ya kununuliwa kwa majokofu hayo wameondokana na tatizo hilo.

Diwani wa Bwawani, Sailon Pashila, aliishukuru serikali kwa kuwaletea vifaa tiba na kuwaondolea adha wananchi ya kwenda mbali kupata huduma za afya hasa upasuaji.

Pashila, alisema kwa sasa wananchi watakuwa wanakwenda katika Hospitali ya Wilaya kupata matibabu endapo itashindikana kwenye kituo hicho.

"Tunaomba serikali ituongeze na watalamu wa afya ili huduma ziweze kutolewa kwa wakati na kwa ufanisi zaidi," alisema Mpashila.

Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Edward Tengulaga, alisema vifaa vilivyopokelewa vina thamani ya Sh. milioni 212 baada ya serikali kutoa fedha za kununulia MSD.

Tengulaga, alivitaja baadhi ya vifaa hivyo kuwa ni vitanda 70, magodoro 70, kitanda kimoja cha upasuaji na kipimo cha Utra Sound. "Tunategemea kupokea vifaa vingine kabla ya Machi 15, mwaka huu na kuanza kutoa huduma za upasuaji na nyingine tunaendelea nazo kama kawaida," alisema.

Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Linus Mwanitega, alisema vifaa tiba vilivyopokelewa vitasaidia kutatua kero za wananchi ikiwa ni pamoja na huduma za upasuaji.



# Wizara ya Utalii yajizatiti kushirikiana na sekta binafsi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale imesema katika kutangaza sekta ya utalii itahakikisha inashirikiana na sekta binafsi ili kufikia malengo katika masoko.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, wakati akitoa ufafanuzi wa mikakati ya serikali katika kutangaza sekta ya utalii kwa kuwashirikisha wadau sekta binafsi.

Alisema yamekuwepo mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka mitatu ya kutangaza utalii nje ya nchi, ambapo mabara yote yaliyopo duniani yamefikiwa.

Alisema sekta binafsi ikiwemo ZATI pamoja na ZATO wanashiriki kikamilifu katika kutangaza sekta ya utalii na kutoa mfano wa hivi karibuni wa maonesho ya utalii yaliyofanyika Zanzibar.

Mudrik alisema wadau hao wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kutangaza utalii pamoja na kuleta watalii nje ya nchi, hatua ambayo inakwenda sambamba na malengo ya SMZ ya kupokea watalii.

"Mheshimiwa Spika tumepiga hatua kubwa katika kutangaza utalii nchini ambapo tunawashirikisha wenzetu sekta binafsi ambao huleta watalii katika pembe zote za dunia"alisema.

Aidha Soraga alizipongeza ofisi za ubalozi wa Tanzania zilizopo nje ya nchi kwa kufanya kazi kubwa ya kuitangaza Zanzibar katika sekta ya utalii.

Alisema hatua hiyo imesaidia Zanzibar kushiriki kikamilifu katika maonesho mbalimbali yanayofanyika nje ya nchi na kutangaza sekta hiyo.

Alisema: "Mheshimiwa nachukuwa nafasi hii kuzipongeza ofisi zetu za ubalozi zilizopo nje ya nchi kwa kazi kubwa wanayoifanya kutangaza utalii wetu zaidi katika kipindi cha maonesho ya kimataifa".



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Juma Makungu akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali kuwapa 'shavu' makandarasi wazawa katika miradi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Fedha na Mipango, Juma Makungu Juma, amesema Serikali itaendelea kuwashirikisha makandarasi wazawa katika kuwapa kazi mbalimbali za miradi ya ujenzi kwa kutumia vigezo vya ushindani wa kibiashara.

Aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Abdalla Ameir aliyetaka kujuwa kwa kiasi gani serikali inatoa nafasi ya kuwashirikisha makandarasi wazawa kuwapa kazi za miradi.

Makungu alisema kwa mfano zabuni za miradi ya kimkakati zilitangazwa hadharani na makandarasi mbalimbali waliwasilisha maombi yao ikiwemo wazawa na wapo waliotunukiwa kazi hizo.

Alisema jumla ya kampuni tisa za wazawa zilipata kazi za ujenzi wa miradi ikiwemo masoko, shule za sekondari pamoja na hospitali za wilaya 11 za Unguja na Pemba.

Aliitaja kampuni ya Quality Building ilipata kazi ya kujenga Hospitali ya Kitogani Wilaya ya Kusini Unguja wakati kampuni ya Qiro ikipewa kazi ya kutengeneza boti 577 aina ya fiber kwa ajili ya wakulima wa mwani.

Aidha alisema Mazuri Building Contract ilipewa kazi ya mradi wa ujenzi wa Shule ya Mjumuisho ya Pujini Pemba pamoja na Hospitali ya Kivunge Wilaya ya Kaskazini Unguja.

Akifafanua zaidi alisema kampuni ya Mwamba ilipewa kazi ya ujenzi wa Shule ya Mjumuisho ya Jendele Wilaya ya Kati Unguja wakati kampuni ya Kimbilio ilipewa kazi ya kukamilisha Shule ya Sekondari ya Bweleo Unguja.

Kampuni nyingine za kizalendo zilizopewa kazi katika miradi mbalimbali ikiwemo Comfix iliyopewa kazi ya kufunga mashine za kiwanda cha usarifu wa samaki sambamba na kampuni ya Amos iliyopewa kazi ya kusambaza boti za uvuvi zipatazo 75.

Alisema: "Mheshimiwa Spika hizo ni baadhi ya kampuni za watu binafsi ambazo zilipewa kazi za miradi mbali mbali ya serikali ikiwemo inayotokana na fedha za uviko 19 na kuzitekeleza kwa umakini mkubwa".

# Serikali kuipa kipaumbele miradi ya kimkakati

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itahakikisha miradi ya kimkakati inatekelezwa kwa wakati kwa lengo la kuleta mageuzi makubwa, ikiwemo miradi ya kukifungua Kisiwa cha Pemba kiuchumi na uwekezaji.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk.Khalid Salum Mohamed katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi kuhusu miradi ya kimkakati inayotekelezwa katika Kisiwa cha Pemba ikiwemo ya ujenzi wa Barabara ya Chake hadi Wete na ujenzi wa Bandari ya Wesha pamoja na Wete Pemba ambayo imetajwa katika ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Dk. Mohamed alisema mikakati ya serikali ni kukifunguwa Kisiwa cha Pemba kiuchumi na uwekezaji kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati.

Aliutaja mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba ambao tayari utekelezaji wake umeanza katika hatua tofauti na unatajwa kuleta mageuzi makubwa katika Kisiwa cha Pemba katika huduma za usafirishaji abiria na kuingiza idadi kubwa ya watalii.

"Mheshimiwa Spika nataka niwajulishe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tunatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba ambapo mkandarasi kwa sasa ameanza kazi na mambo mengine ya msingi yaliyobakia yamekamilika ikiwemo kulipa fidia mali za wananchi ili kupisha ujenzi" alisema.

Aidha alisema katika Kisiwa cha Pemba serikali inatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa Bandari ya Wesha pamoja na Wete ambazo zitaunganisha Kisiwa cha Pemba na mikoa jirani ya Tanzania Bara hadi Mombasa Kenya.

Kuhusu Bandari ya Wete alisema tayari upembuzi yakinifu unaendelea kuona aina ya ujenzi wa bandari hiyo utakavyofanyika na kuweza kutoa huduma kwa wananchi wa Pemba na mikoa jirani.

"Tunafanya upembuzi yakinifu ambapo kampuni inayofanya kazi hiyo inaendelea kuona aina ya bandari hiyo itakayojengwa ambapo tunafahamu Bandari ya Wete ni muhimu ikiwa ni kiungo cha mikoa jirani ya Tanzania Bara na Mombasa Kenya" alisema.

Alisema katika sekta ya barabara serikali inafuatilia kwa karibu miradi yote inayotekelezwa kwa sasa ikiwemo ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete, pamoja na barabara zinazokwenda katika maeneo huru ya uchumi Micheweni.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**NEEMA CHARLES LYIMO** MTAJWA HAPO JUU AMEPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE MAENEO YA KISESA MWANZA. **INDEX NO; S1334/0023,** SHULE; **MHONGOLO PROGRESSIVE SECONDARY SCHOOL** MWAKA: 2017, TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KITUO CHA POLISI KISESA RB NA. **PHQ/MWA/MAG/4764/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**BENEDICTO LAURENT MBONYE** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma; cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1489/0094** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia SHULE YA KATUBUKA SEKONDARI mwaka 2018, na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.10798/1032** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia SHULE YA SEKONDARI KOROGWE mwaka 2021 na cheti cha diploma chenye namba ya usajili **E.505/0486** kilichotolea na CHUO CHA UALIMU KOROGWE mwaka 2022. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **KGT/RB/178/2023, KGT/RB/179/2023, KGT/RB/180/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA**

**KUITWA SHAURINI**

**MADAI NO.65/2022**

**MDAI: TATA AFRICAN COMPANY LTD AND ONE ANOTHER**

**MDAIWA AGROFRESH COMPANY LTD.**

Madai hayo yamefunguliwa katika mahakama hii Ndugu **AGROFRESH COMPABY LTD**
Unaamriwa na mahakama hii kuhudhuria mnamo tarehe 01/03/2024na usipohudhuria shauri litasikilizwa upande mmoja na uamuzi kutolewa.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA TEMEKE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER MATHIAS MASSAWE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **CANTER** yenye usajili namba **T 606 AWW** na CHASSIS NAMBA: **FF315BD513917.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/KIN/40458/2023**

## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI

**JOSEPHINE JOSEPH MAKAMBA** anatangaza kupotea kwa kadi za bajaji zenye usajili namba: **MC 911 DAY, MC 443 BSF, MC 331 BPT na TJ 06 AWU.**kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**KMR/RB/109/2024**

## WITO WA KIKAO CHA MIRATHI YA MZEE ALEXANDER ITAELI KWEKA

Wasimamizi wa Mirathi ya ***Mzee Alexander Itaeli Kweka*** **,** Wanaitisha na kuwakaribisha Warithi na Wana ukoo wa Kweka katika kikao muhimu kitakachofanyika **Bomangombe HAI MOTEL GARDEN (PAPAA)** siku ya **jumamosi tarehe 09/03/2024, saa nne asubuhi.**

**TAFADHALI WAHI NA FIKA BILA KUKOSA**

**ASANTENI SANA.**

**Notice of date of hearing to plaintiff and Respondent**

**IN THE DISTRICT COURT OF MBOZI DISTRICT AT VWAWA**

**MATRIMONIAL/ CIVIL APPEAL NO 834 OF 2024**

**BANK OF AFRICA TANZANIA LIMITED PLAINTIFF(S)**

**VERSUS**

**VICTOR CHARLES NGAILO ..................RESPONDENT**

**TO VICTOR CHARLES NGAILO**

**TAKE NOTICE THAT** the above mentioned civil case has been fixed for mention/hearing on 06th MARCH day of 2024 and you are required to enter appearance at such time and date.
**AND TAKE FURTHER NOTICE THAT,** if you default to enter appearance as aforesaid in the case and be determined in your absence.
Given under my hand and the seal of the court this 21 day of 2 ...2024

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE INCHARGE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA KATA NSHAMBYA BUKOBA**

## WITO

**POPOTE ULIPO**

WEWE ANNA GRATION UNATAKIWA KUFIKA MBELE YA BARAZA HILI TAREHE 5/3/2024 SIKU YA JUMANNE SAA 2:30 ASUBUHI. FIKA BILA KUKOSA WALA KUCHELEWA, USIPOFIKA HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YAKO.

MWENYEKITI
..............................
*BARAZA LA KATA NSHAMBYA*

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 3394 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late: EDIFONSIA NICAS NYOVU**

**By 1: NICAS EMMANUEL NYOVU**
**2: __________________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 14 day of 3.2024
Dated at 22 this 02 day of 2024

RESIDENT MAGISTRATE

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***
***Kwa Bei Poa***
***Tupigie +255 - 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Vikosi vya usalama Chad vyachunguza shambulizi

**N'Djamena,** Chad

VIKOSI vya usalama nchini Chad vimefanya upekuzi wa dharula kwa magari na watu katika mji mkuu wa N'Djamena baada ya kusikika milio ya risasi karibu na makao makuu ya chama kikuu cha upinzani.

Tukio hilo lilitokea jana baada ya kutokea ufyatulianaji risasi karibu na makao makuu ya chama kikuu cha upinzani cha Socialist Party Without Borders (PSF).

Awali serikali iliwatuhumu wanachama wa upinzani kuhusika na tukio la watu kadhaa kuawa katika shambulizi kwenye ofisi ya idara ya usalama wa ndani.

Kiongozi wa chama cha PSF, Yaya Dillo ambaye ni mpinzani mkubwa wa Rais wa Mpito wa Chad, Mahamat Idriss Deby Itno, alikanusha kuhusika katika shambulizi hilo lililofanyika Jumanne usiku. Akizungumza na shirika la habari la Ufaransa ( AFP), Dillo ambaye pia ni binamu wa Deby, alizitaja shutuma hizo kama za uwongo na kueleza hakuwepo wakati tukio hilo linatokea.

Alisema lengo la serikali ni kumzuia na kumtisha ili asigombee nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Mei 6, mwaka huu.

Shambulizi hilo lilifanyika siku moja baada ya kutangazwa tarehe ya uchaguzi ambao utawakutanisha ndugu hao. **RFI**

# Rais Putin azikosoa nchi za magharibi

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia , Vladimiry Putin amezikosoa nchi za Ulaya na kuzitaja kama mataifa yaliyoshindwa.

Katika hotuba yake Putin, alisema nchi za Magharibi zilitaka kuunda na kuharibu nchi yake, badala yake wao ndio wamepoteza.

Putin aliendelea kuisifu Russia na watu wake kuwa kwa karne nyingi wameishi katika umoja na kuunda nguvu isiyoweza kushindwa.

Alisema kwamba Russia ni nguzo ya demokrasia na hataruhusu mtu yeyote kuingilia masuala yake ya ndani.

Hotuba hiyo ameitoa wiki moja baada ya kifo cha Alexei Navalny, ambaye ni mmoja wa wapinzani wakubwa wa Putin.

Familia ya Navalny inamtuhumu Putin kwa kupanga kifo chake, jambo ambalo Ikulu ya Kremlin inakanusha. **BBC**

# Watoto wazidi kuuawa Gaza

**GAZA,** Palestina

SHIRIKA la kimataifa linalotetea haki za watoto la Save the Children, limesema mauaji ya kutisha ya watoto yanaendelea katika Ukanda wa Gaza wakati jeshi la Israeli likipambana na kundi la Hamas.

Mkuu wa shirika hilo anayehusika na masuala ya sera, Alexandra Saieh, alisema kinachoendelea katika eneo hilo ni mauaji ya holela ya watoto yanayoendelea kushuhudiwa.

Kauli hiyo inakuja wakati wizara ya afya katika ukanda wa Gaza, ikisema watoto sita wameuawa kaskazini mwa eneo hilo kwa kukosa maji na utapiamlo, na wengine hali zao za kiafya ni mbaya.

Umoja wa Mataifa umeonya kuwa, watu zaidi ya 500,000 wapo kwenye hatari ya kupoteza maisha kutokana na janga la njaa kufuatia misaada ya kibinadamu kutowafikia wakazi wa Gaza walioathiriwa na vita vinavyoendelea.

Katika hatua nyingine, idadi ya vifo vinavyotokana na vita vinavyoendelea imeongezeka na kufika zaidi ya elfu 30 kwa mujibu wa wizara ya afya kwenye ukanda wa Gaza.



Watu wanaoshukiwa kuwa ni wahalifu wakiwa chini ya ulinzi baada ya operesheni maalumu ya polisi kufanyika Januari 18, mwaka huu. Picha hiyo ilichukuliwa katika gereza namba 8 katika mji wa Guayaquil nchini Ecuador. **PICHA: AFP**

# Biden,Trump watunishiana misuli, kila mmoja ashinda Michigan

**WASHINGTON,** Marekani

KINYANG'ANYIRO cha uchaguzi wa rais nchini Marekani kinazidi kuwa kigumu baada ya Rais Joe Biden na mtangulizi wake Donald Trump, kushinda katika chaguzi za awali katika jimbo la Michigan.

Rais Biden kutoka chama cha Democrats na Trump wa Republican wote wawili wameshinda katika uteuzi wa vyama vyao kugombea katika uchaguzi wa mwezi Novemba.

Biden alishinda kirahisi uchaguzi wa awali wa chama chake cha Democratic katika jimbo la Michigan, lakini kura ya upinzani iliyopigwa na baadhi ya wanachama wa chama hicho wenye ghadhabu kutokana na hatua ya kiongozi huyo kuunga mkono vita vya Israel dhidi ya Hamas katika Ukanda wa Gaza, uliwashtua waandaaji wa uchaguzi huo.

Katika jimbo la Michigan ambalo lina idadi kubwa ya Wamarekani wenye asili ya kiarabu, wapiga kura wa chama cha Democratic walihimizwa waandike katika kura zao kwamba hawajaamua kujitolea kumuunga mkono Biden katika hatua ya kupinga sera kuhusu vita vya Gaza. Haikufahamika ni kura ngapi zilizoandikwa maneno hayo.



Biden



Trump

Wamarekani wengi wenye asili ya kiarabu wanaoishi Michigan walimuunga mkono Biden mwaka 2020.

Hata hivyo, wameghadhabishwa na hatua ya Biden kuunga mkono harakati ya kijeshi ya Israel katika Ukanda wa Gaza unaotawaliwa na Hamas, ambako maelfu ya Wapalestina wameuliwa.

Mwakilishi wa jimbo la Michigan wa chama cha Democratic, Abraham Aiyash, alisema wasijaribu kubadilisha maelezo baada ya usiku wa jana kwamba chama hicho kina mpasuko.

"Tunajaribu kukiokoa chama cha Democratic kutokana na mauaji ya halaiki. Tunajaribu kukiokoa chama cha Democratic kutokana na ukiukaji wa haki za binadamu na kutojali ubinadamu wa ndugu na dada zetu Wapalestina." alisema

Waandaaji wa kampeni waliapa kuwasilisha ajenda yao ya kupinga vita kwenye mkutano mkuu wa chama utakaofanyika Agosti mjini Chicago.

Kwa upande mwingine,rais wa zamani Donald Trump ameshinda uchaguzi wa awali wa chama cha Republican kwa kura nyingi katika jimbo hilo la Michigan.

Kutokana na ushindi huo ameimarisha nafasi yake ya kushinda uteuzi wa chama hicho huku akimuacha mbali katika nafasi ya pili mpinzani wake wa mwisho aliyebaki, Nikki Halley.

Baada ya ushindi huo Trump alisema Novemba jimbo hilo la Michigan litamwambia Joe Biden kuwa mpotovu, na atatimuliwa madarakani.

Trump sasa ameshinda katika majimbo yote matano ya kwanza katika kalenda ya uchaguzi wa awali wa chama cha Republican.

Ushindi wa Trump dhidi ya mpinzani wake Nikki Haley, unakuja baada ya rais huyo wa zamani kumshinda kwa asilimia 20 katika jimbo lake la nyumbani la South Carolina Jumamosi iliyopita.

Timu ya kampeni ya Trump inapania kupata kura za wajumbe 1,215 zinazohitajika kushinda uteuzi wa chama cha Republican kufikia katikati ya Machi. **DW**

# WASANII Z'BAR WATAKIWA KUCHANGAMKIA FURSA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imewataka wasanii visiwani hapa kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza ili kukuza kazi zao za sanaa na kujiongezea kipato.

Akizungumza katika hafla maalum ya kutaja vipengele na Wasanii watakaowania tuzo za kimataifa za muziki za Zanzibar 'Zanzibar International Music Awards (ZIMA) zinazotarajiwa kutolewa Aprili 27 mwaka huu, Waziri wa Wizara hiyo, Tabia Maulid Mwita, alisema wasanii Wazanzibar hasa wa Muziki lazima wajiongeze na kutanua wigo wa kazi zao.

Alisema anatamani kuona wasanii wa Zanzibar wanafanya vizuri katika kazi zao za Sanaa ikiwa pamoja na kuchangamkia fursa zinazotolewa na Wizara hiyo ambayo inafanya jitihada kubwa kuona sanaa ya Zanzibar inapiga hatua.

**Alisema lengo la kuanzishwa tuzo hizo ni kuwapa moyo na hamasa wasanii wa Zanzibar ili kufanya sanaa yao kwa malengo na kutumia tuzo hizo kama chachu kwao.**

"Natamani kuona wasanii wa Zanzibar wanashinda vipengele ambavyo wametajwa lakini pia kuona wasanii wanachangaamkia fursa hii kwani hii ni moja ya sehemu ya kuwatia moyo na kuchochea mafanikio yao", alisema Tabia.

Aidha, aliwapongeza wasanii wote wa Zanzibar ambao wameingia katika tuzo hizo na kutaka mchakato wa upigaji kura uwe wa wazi ili kuepusha malalamiko ambayo yanaweza kujitokeza.

Amelitaka Baraza la Sanaa Zanzibar, Sensa ya Filamu na Utamaduni kukutana na vikundi vyama utamaduni vilivyopo ili kukusanya taarifa ya kutopeleka kazi zao kwa kamati ya tunzo hizo licha ya kupewa taarifa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa shirika la utangazaji Zanzibar Ramadhani Bukini ambae ni Mwenyekiti wa Kamati ya tuzo hizo alisema Wasanii watashinda kwenye jumla ya vipengere 24 tofauti.

Alisema hapo awali kamati hiyo ya tuzo ilipendekeza vipengele 28 ambapo vipengele vinne vimeondolewa kwa kutopokea kazi za wasanii.

Akitaja vipengele vilivyofutwa ni Kikundi bora cha utamaduni, Msanii bora wa utamaduni, Mnenguaji bora wa kike wa muziki wa dansi wa mwaka na mnenguaji bora wa Kiume muziki wa dansi.

Alisema kamati ilipitisha vipengele 24 kwa kufuata mchakato sahii ikiwemo kushirikiana na Baraza la Sanaa hapa Zanzibar pamoja na lile la Tanzania Bara (Basata) pamoja na wasanii wenyewe.

"Tulianza mchakato huu mapema pale tu Waziri wa habari alipotaka kuwepo na tuzo za muziki za Zanzibar, mchakato uliwahusisha watu mbalimbali, Wasanii, waandaaji wa muziki na Ma Dj lengo ni kuona tunashirikiana katika kukamilisha kazi hii kwa ubunifu mkubwa" Alisema.

Alisema mchakato wa kuwapigia kura wasanii hao utaanza leo saa sita kamili usiku kupitia code ya kila Msanii.

## Wacheza gofu 80 washirki Lina PG Tour

**Na Mwandishi wetu**

ZAIDI wa wachezaji 80 wameanza kushiriki mashindano ya mchezo wagofu ya Lina PG Tour katika viwanja vya TPC Moshi yakiwa na lengo la kumuenzi mchezaji wa zamani wa timu ya taifa ya mchezo huo, Lina Nkya.

Mashindano hayo yaliyoanza jana yanafanyika mkoani Kilimanjaro yameandaliwa na familia ya Nkya kwa kushirikiana na Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU).

Lina Nkya enzi ya uhai wake alikuwa mchezaji wa Timu ya Taifa ya Gofu na miongoni mwa wachezaji waliopeperusha vyema bendera ya Tanzania mwaka 2011 walipotwaa taji la Afrika Mashariki na Kati katika mashindano yaliyofanyika Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa usajili wa wachezaji hao Makamu wa Rais wa TLGU, Ayne Magombe, alisema kati ya wachezaji hao 80 waliojitokeza, wapo wachezaji wa kulipwa 16 ambao wamejitokeza kushiriki.

Alisema ushiriki wa wachezaji hao umeonyesha namna watu walivyokuwa wanamkubali mchezaji huyo wa zamani hivyo anategemea ushindani utakuwa mkubwa.

"Wachezaji wengi wameshawasili na wako tayari kupambana, tunategemea ushindani utakuwa mkubwa na tutaona vipaji vingi, tunawahimiza mashabiki wa mchezo huu kujitokeza kushuhudia mastaa wakichuana,"alisema Magombe



Kijana akipiga mpira wa Tenis kurudisha kwa mpinzani wake wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya Gmykhana jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Bondia Kidunda kumlipia kisasi Twaha Kiduku?

**Na Saada Akida**

SIKU ambayo ilikuwa ikisubiriwa na mashabiki wengi wa ngumi hatimaye imefika ambapo leo bondia Seleman Kidunda atapanda ulingini kupigana na mpinzani wake kutoka Afrika Kusini Asemahle Wellem na swali ambao wadau wa mchezo huo wanalo ni je, Mtanzania huyo ataweza kulipa kisasi?.

Ikumbukwe Wellem kutoka Afrikaalitoa kipigo kwa bondia mwingine wa Tanzania, Twaha Kiduku kwa kumpiga kwa pointi mwaka jana jijini Dar es Salaam.

Awali Kidunda alisema pambano hilo ni muhimu kwake kwa ajili ya kuurejesha Tanzania mkanda wa WBF lakini pia anataka kushinda hili kumlipia kisasi Kiduku.

Pambano hilo la raundi 12 la kuwania mkanda wa WBF linafanyika leo kwenye ukumbi wa Ware House, Masaki, jijini Dar es Salaam ambapo Wellem anatetea mkanda huo alioupata mwaka jana baada ya kumpiga Kiduku.

Kidunda aliiambia Nipashe jana kuwa yupo tayari kwa ajili ya pambano hilo na amefanya maandalizi yakutosha kumkabili Msauzi huyo.

"Sitowaangusha Watanzania, nimejiandaa vizuri na nina uhakika nitafanya vizuri, kikubwa naomba watu wajitokeze kwa wingi kushuhudia nikitoa kipigo," alisema Kidunda.

Kabla ya Kidunda kupanda ulingoni, pia kutakuwa na mapambano mengine ya utangulizi ambapo bondia mwingine Mtanzania, Nassib Ramadhani atapigana na Emmanuel Nadjala kutoka Malawi.

Aidha, Hamad Furahisha atapigana na Ally Mwerange, Lupakisyo Shoti atapigana na Jacob Maganga, Salim Jengo atapanda ulingoni kucheza na Gray Chimkwapulo kutoka Malawi.

Aidha, Mohammed Hamad atazichapa na Aidin Muzei kutoka Uganda, Omary Sultan atapigtana na Salim Athuman, Loren Japhet atapanda ulingoni kuzichapa na Hillary Katuya kutoka Zambia.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa kampuni ya Fay Heroes wanaoandaa mapambano hayo, Abdul Salim alisema maandalizi yamekamilika na mabondia wote kutoka nje ya nchi na mikoani wameshafika Dar es salaa tayari kwa pambano la leo.

## ZISIKUPITE

### SPURS YASAKA KIUNGO

KLABU ya Tottenham Hotspur inawasaka viungo katika usajili wa majira ya joto, huku winga wa Wolves na Ureno, Pedro Neto, 23, na winga wa Crystal Palace na England, Eberechi Eze, 25, wakiwaniwa kwa sasa. ***(Independent)***

### LIVER YAJITOSA KWA ALONSO

LIVERPOOL imewasilisha ombi la awali la kuzungumza na kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso wakitafuta mbadala wa Jurgen Klopp anayeondoka. ***(Bild)***

### HATIMA YA GREENWOOD

MANCHESTER United itafanya uamuzi kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa England, Mason Greenwood, 22, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Getafe, ifikapo mwisho Mei. ***(Sun)***

### RAMAJ ASAKWA EPL

ARSENAL, Manchester United na Chelsea zina nia ya kumsajili golikipa wa Ujerumani, Diant Ramaj, 22, kutoka Ajax. ***(Bild)***

### ALLI MKATABA MPYA

MAISHA ya Dele Alli, 27, pale Everton yanaweza kuwa mazuri baadaye mwaka huu kwa vile klabu hiyo iko tayari kumpa mkataba mpya kiungo huyo wa zamani wa England. ***(Express, via Athletic)***

### SON KUONGEZEWA SPURS

MSHAMBULIAJI wa Korea Kusini, Son Heung-min, 31, anameridhika Tottenham Hotspur na mazungumzo rasmi kuhusu mkataba mpya yamepangwa kuanza. ***(Football Insider)***

### LEAO HAONDOKI MILAN

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 24, amekuwa akihusishwa na Barcelona, lakini anasema "hawezi kuondoka" AC Milan. ***(Sport)***

### JORGINHO KUREJEA SERIE A

KIUNGO wa kati wa Italia, Jorginho mwenye umri wa miaka 32 anaweza kurejea Serie A mkataba wake na Arsenal utakapokamilika msimu huu wa majira ya joto. ***(Goal)***

### NYOTA WAWANIA SAUDIA

KLABU za Ligi Kuu ya Saudi Arabia zinawanyatia nyota kadhaa wa Ligi ya England katika usajili wa majira ya joto, wakiwemo wachezaji wachanga kama vile mshambuliaji wa Argentina, Matias Soule mwenye umri wa miaka 20, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Frosinone kutoka Juventus. ***(ESPN)***

### ROBERTO ANAITAKA MLS

TIMU ya daraja la pili ya Saudi Arabia ya Al Qadsiah ilitoa ofa nono kwa kiungo wa zamani wa Hispania, Sergi Roberto, lakini nahodha huyo wa Barcelona mwenye umri wa miaka 32 angependelea kuhamia Ligi Kuu ya soka ya Marekani MLS. ***(Mundo Deportivo)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# BARCELONA YAJITOSA KUMUWANIA DE GEA

**Golikipa huyo amebaki bila timu baada ya kuondoka Manchester United majira ya...**

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inafikiria kumsajili golikipa, David de Gea ambaye ni mchezaji huru, kwa mujibu wa ripoti.

**De Gea amebakia bila klabu baada ya kuondoka Manchester United majira ya joto yaliyopita wakati mkataba wake ulipoisha.**

Hapo awali alikuwa amekubali masharti ya mkataba mpya Old Trafford hadi klabu ilipoghairi ofa hiyo na kujaribu kumpa mkataba mpya kwa malipo ya chini, na Mhispania huyo hatimaye kuamua kuondoka baada ya miaka 12 ya kukaa klabuni hapo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 amebakia bila klabu na mechi yake ya mwisho ya ushindani ilikuwa United ilipofungwa 2-1 na wapinzani wao Manchester City kwenye fainali ya Kombe la FA Juni mwaka jana ambapo alikosolewa kwa kufungwa mabao yote mawili.

Lakini sasa gazeti la Katalunya la Mundo Deportivo limeripoti kwamba hivi karibuni anaweza kurejea kwenye soka akiwa na Barcelona.

La Blaugrana hao wamebakia na matatizo ya kifedha, walitumia euro milioni 3.4 pekee katika ada za uhamisho msimu uliopita wa joto, huku gharama yao ya msimu wa baridi ya euro milioni 40 ilitumika kumnunua fowadi wa Brazil, Victor Roque na wanaona kusajiliwa bila malipo kwa De Gea kama ni suluhu la gharama nafuu.

Mlinda mlango wa sasa Marc-Andre ter Stegen amekuwa akihusishwa na kuhamia Saudia katika wiki za hivi karibuni, huku Inaki Pena akicheza vizuri msimu huu na huenda akakabiliwa na nia ya kuhama.

Katika hatua hii, kuna uwezekano mkubwa kwamba De Gea atatumika mbadala wa Ter Stegen.

De Gea alikuwa kwenye mazungumzo juu ya kuhamia kwa wapinzani wa Barcelona Real Madrid msimu uliopita wa joto baada ya Thibaut Courtois kupata jeraha, lakini wakachagua kumsajili Kepa Arrizabalaga kwa mkopo kutoka Chelsea badala yake.

Bayern Munich vile vile walikuwa kwenye soko la kutafuta golikipa msaidizi na walimfikiria De Gea kabla ya kumgeukia mchezaji wa kimataifa wa Israel, Daniel Peretz.

Klabu ya Nottingham Forest na Al Shabab inayoshiriki ligi kuu ya Saudi Arabia zote zilikuwa na nia ya kumsajili De Gea wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari, lakini hatua hizo hazikutimia.

## HABARI MICHEZO

# TEN HAG: KILA USHINDI NI MUHIMU




**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag aliwasifu wachezaji wake wa Manchester United baada ya kupata ushindi wa 1-0 kwenye uwanja wa Nottingham Forest na kutinga robo fainali ya Kombe la FA, Jumatano.

Bao la kichwa la dakika za lala salama lililofungwa na Casemiro kutokana na krosi ya faulo ya Bruno Fernandes liliwafanya Mashetani Wekundu hao kupita hatua ya nane bora, ambapo watacheza na wapinzani wao Liverpool. Ushindi huo pia ulikuwa njia muafaka ya kujikwamua kutokana na kichapo cha 2-1 Jumamosi iliyopita dhidi ya Fulham kwenye uwanja wa Old Trafford.

Lakini licha ya shinikizo lililotokana na matokeo hayo ya mshtuko, Ten Hag alikuwa muhimu kuzungumzia uthabiti wao.

Bosi huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 54, aliambia BBC: "Kila ushindi ni muhimu. Tunachukua saa 24 kisha tunaendelea.

"Michezo ya ajabu inakuja. Timu hii, walichokionyesha leo, ni kizuri sana. Wanapaswa kuonesha kila mchezo. Nimeiona miezi michache iliyopita, sio Jumamosi.

"Tulipata njia ya kushinda. Tulikuwa thabiti. Tulipoteza mara moja mnamo 2024. Tuko thabiti.

"Siyo rahisi sana unapokuwa na safu nzima ya nyuma na inabidi tuchanganye na kucheza wachezaji katika nafasi tofauti. Ninajivunia tulifanya hivyo."

Ten Hag pia alifurahishwa sana na jinsi Casemiro alivyofunga bao la ushindi, huku United wakipiga mashuti saba yaliyolenga lango muda wote wa mchezo.

Hata hivyo, kocha huyo wa United alijua timu yake ilisalimisha nafasi nyingi mno huku Forest ikipiga mashuti 16 licha ya kuwa na asilimia 39 pekee ya umiliki wa mpira.

## Kroos aelezea sababu kurudi kimataifa

**MADRID,** Hispania

KIUNGO wa kati wa Real Madrid, Toni Kroos amesema "sikuwahi kutilia shaka uamuzi wangu" kurudi kucheza soka la kimataifa ili kuiwakilisha Ujerumani kwenye michuano ya Euro 2024.

Kroos aliachana na majukumu ya kimataifa karibu miaka mitatu iliyopita baada ya michuano ya Euro 2020 iliyokatisha tamaa.

Ujerumani tayari ilikuwa na wakati mbaya kwenye Kombe la Dunia 2018 iliposhindwa kutoka katika hatua ya makundi, kisha ikarudia makossa hayo mwaka 2022 bila Kroos.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 alithibitisha wiki iliyopita kuwa atarejea katika kikosi cha Ujerumani mwezi ujao.

Akienda kwa undani zaidi kuhusu uamuzi huo, Kroos alieleza kwenye podikasti yake ya Einfach mal Luppen: "Hakujawa na wakati ambapo nilitilia shaka. Pengine isingekuwa vyema kusema hivyo sasa, lakini ni kweli kutoka chini kabisa ya moyo wangu.

"Ningesema kwamba nilifikiria kila kitu vizuri. Nilichukua muda wa kutosha kufikiria kila kitu na nikafikia hitimisho kwamba nafasi bado ninayo."

Ujerumani itakuwa kwenye ardhi ya nyumbani msimu wa joto, wakitaka kushinda taji la kwanza la kimataifa tangu Kombe la Dunia mwaka 2014. Mafanikio yao ya mwisho ya Ubingwa wa Ulaya yalikuja mwaka 1996.

Kuhusu mustakabali wa klabu yake, Kroos ana mkataba na Real Madrid hadi Juni. Hakusaini mkataba huo hadi mkataba wake wa awali ukiwa umesalia siku chache kumalizika msimu uliopita wa joto na anaweza tena kuchelewesha uamuzi wowote kuhusu msimu ujao hadi mwishoni mwa msimu, au hata baada ya mkataba wake kumalizika.






## *Liver haina wasiwasi kumkosa Alonso*

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL haina wasiwasi kuhusu uwezekano wa kumpoteza mlengwa wao mkuu wa ukocha, Xabi Alonso kwenda Bayern Munich, kwa mujibu wa 90min.

Liverpool na Bayern zote zinasaka kocha mpya huku mabosi wao wa sasa wakitarajiwa kujiuzulu mwishoni mwa msimu huu.

Jurgen Klopp alithibitisha kuondoka kwake Anfield Januari baada ya kufanya uamuzi kwa faragha Novemba, huku Thomas Tuchel akiondoka Allianz Arena majira ya joto.

90min hivi majuzi iliripoti kuwa anayeongoza orodha ya makocha saba wanaowaniwa na Liverpool kuchukua nafasi ya Klopp ni Alonso, ambaye yuko mbioni kuiongoza Bayer Leverkusen kutwaa taji lao la kwanza kabisa la Bundesliga msimu huu.

Lakini Bayern sasa pia wako sokoni kutafuta kocha na Alonso ndiye mgombea mkuu kuchukua mikoba ya pale Bavaria. Licha ya hayo, vyanzo vimeiambia 90min kwamba Liverpool hawajashtushwa na maslahi haya ya wapinzani na wanaamini kuwa wanadhibiti hali hiyo.

Hisia za Liverpool ni kama hawatamchukua Alonso, itakuwa ni kwa sababu wana mgombea mwingine akilini mwao kwa kazi hiyo badala yake wekundu hao wanatarajia kuteua Mkurugenzi mpya wa michezo katikati ya mwezi Machi kabla ya kukamilisha kuajiri kocha.

Inachukuliwa kuwa muhimu Mkurugenzi wa michezo kuja kwanza, na labda hata aina tofauti ya muundo na safu ya majukumu mapya ya kuajiri na vyeo.

## HABARI MICHEZO

# BITEKO ATAKA WASANII KUTHAMINIWA, KULIPWA

**Na Saada Akida**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk Dotto Biteko ametoa maagizo kwa Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk Damas Ndumbaro kuhakikisha wasanii wanalipwa kwenye shughuli za kiserikali wanazoshiriki kutoa burudani.

**Aidha, Dk Biteko ametaka Wasanii wathaminiwe na kupewa heshima zao kutokana na kazi kubwa wanayoifanya ya kuelimisha na kuburudisha jamii.**

Dk Biteko aliyazungumza hayo jana kwenye Mkutano wa Wadau wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa uliofanyika jana akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk Samia Suluhu Hassan ambaye alikuwa mgeni rasmi.

Dk Biteko alisema Wizara inatakiwa kuwaona Wasanii kama nyenzo muhimu katika Taifa kwa sababu Sanaa ni kuelimisha, kuburudisha na sasa imekuwa ajira kwa vijana wengi wa Tanzania.

Alisema Waziri anayeshughulikia sanaa anapaswa kuwa daraja la kuunganisha wasanii katika kupata kazi ikiwemo katika kampeni, matukio ya Kiserikali na kulipwa kwa kazi zao na sio kupewa neno la 'Asante' peke yake.

"Waziri nahitaji kuona katika shughuli za Serikali Wasanii wanapewa kazi na kulipwa kwa sababu sanaa ni ajira na sio kupewa neno la Asante tu, lakini pia mabenki yarahisishe masharti kwa wasanii kuweza kupata mikopo," alisema Dk Biteko.

Aliongeza kuwa kulijua taifa hupaswi kuhangaika teknolojia, hangaika na utamaduni wake ikiwemo lugha yake na chakula chake.

"Wasanii wana kazi kubwa sana ya kulifanya taifa hili kuwa hai kwa kuenzi utamaduni wa nchi yetu, kusisitiza juu ya utamaduni wetu. Licha ya kuwepo kwa mambo yetu ndani, basi tusikubali kudhalilisha utamaduni wetu kwa mgeni ambaye anakuja kututembelea," alisema Dk Biteko.

Alisema Sekta ya Utamaduni inaongoza kwa ukuwaji kuliko sekta zote nchini kwa sasa imekuwa kwa asilimi 19 lakini imekuwa duni katika mchango wa taifa," alisema Biteko.

Wakati huo huo, Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo Dk Ndumbaro alisema Serikali ipo mbioni kuanzisha mji wa sanaa.

Alisema Rais Samia katika kujali na kuipambania sana alipata nafasi ya kuzungumza na Muigizaji na DJ, Idris Elba wa Uingereza kwa ajili ya kuja kuwekeza nchini.

"Hivi karibuni Rais alipokwenda Uingereza alikutana na Muigizaji huyo hakuna mtu aliyemtuma bali ni mapenzi yake na kutaka kuona Sanaa na Utamaduni wetu unakuwa pamoja na wasanii wetu kukuwa zaidi," alisema Ndumbaro.



Vijana wanaolelewa katika kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam, wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Tabora United haijashinda Ligi Kuu 2024

**Na Adam Fungamwango**

KIPIGO cha mabao 2-1 ilichokipata juzi kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya dhidi ya wenyeji Tanzania Prisons, kimeifanya timu ya Tabora United kuendelea kuweka rekodi ya kutoshinda mechi yoyote tangu mwaka huu uanze.

Ushindi wa Tanzania Prisons unawapeleka hadi nafasi ya tano kwa mara ya kwanza baada ya misimu mingi kupita, ikifikisha pointi 24 baada ya kucheza mechi 18 mpaka sasa.

Mabao ya winga machachari, Zabona Mayombya dakika ya 21 na mshambuliaji Samson Mpangula aliyepachika bao la ushindi dakika mbili kabla ya mechi kumalizika, huku Erick Okutu akifunga bao la kufutia machozi kwa wageni.

Tabora United haijashinda mechi yoyote ya Ligi Kuu tangu Desemba Mosi mwaka jana ilipoifunga Mtibwa Sugar mabao 2-1, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, lakini baada ya hapo imecheza mechi nane bila kupata ushindi, ikifungwa nne na sare nne.

Baada ya ushindi huo wa Desemba Mosi, Ilitoka sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Mashujaa, Desemba 5, ikachapwa mabao 2-1 ugenini dhidi ya Ihefu Desemba 8, kabla ya kufungwa bao 1-0 na Yanga, Desemba 23 kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma, ikiwa ni mechi ya mwisho kwa mwaka jana.

Mwaka huu ilikutana na kipigo cha mabao 4-0 nyumbani dhidi ya Simba, ikatoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo Februari 11, ilitoka suluhu dhidi ya Azam FC, Februari 10 na Jumapili iliyopita ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Singida Fountain Gate kabla ya juzi kupata kipigo mbele ya Tanzania Prisons.

## *Benchikha ambadilishia Kanoute*

INATOKA UKURASA 24

Golikipa namba moja wa Simba, Aishi Manula akizungumzia mchezo huo wa kesho alisema ni mchezo mgumu ambao ni lazima wapate ushindi kuweza kuweka hai malengo yao ya kucheza nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Ni mchezo wa kufa na kupona, ni mchezo ambao wanasimba wote wanauangalia kwa jicho la kufuzu, wachezaji tutapambana na 'Inshallah'., tutapata ushindi, tunaomba mashabiki waje uwanjani kwa wingi kwa sababu uwepo wao utatuongezea hamasa zaidi sisi wachezaji kuweza kuimaliza mechi na kupata ushindi," alisema Manula.

Katika hatua nyingine, Meneja habarina Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally anaendelea na hamasa kwa mashabiki wa timu hiyo kuelekea kwenye mchezo huo muhimu.

Baada ya kuzindua hamasa juzi kwenye tawi la Keko Maduka mawili, jana walikuwa kwenye kituo cha mabasi ya Mwendo kasi cha Gerezani ambapo aliingia kwenye mabasi hayo nakuanza kuhamasisha mashabiki wa timu hiyo mpaka kituo cha mabasi cha Magufuri (Mbezi) ambako tiketi za kuangalia mchezo huo ziliuzwa kwa wingi.

Simba inahitaji ushindi wowote kuweza kufuzu hatua ya robo fainali bila kuangalia matokeo ya Wydad Casablanca ya Morocco ambao wenyewe watacheza na Asec Mimosas kwenye mchezo mwingine wa Kundi hilo.

Matokeo yoyote nje ya ushindi yatatoa nafasi kwa Waarabu hao kutinga hatua ya robo fainali kama watawafunga Asec Mimosas. Hiyo inatokana na timu hizo mbili (Simba na Wydad) kulingana pointi (zote zikiwa na pointi sita), lakini Simba ina faida ya matokeo mazuri baina ya timu hizo mbili 'head to head'.

## Tatu kushiriki 'CRDB Inter club'

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU tatu za mchezo wa gofu zinatarajiwa kushiriki mashindano ya 'CRDB Inter Club Competition' yatakayofanyika Machi 9 kwenye viwanja vya Klabu ya Lugalo jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Waandishi wa Habari jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Meja Selemani Semunyu alisema mashindano hayo yatashirikisha klabu za gofu Morogoro, Dar es Salaam Gymkhana pamoja na wenyeji Lugalo.

Alisema maandalizi kuelekea kwenye mashindano hayo yanaendelea vema na Klabu zote zimethibitisha ushiriki wa mashindano hayo.

" Maandalizi kuelekea kwenye mashindano haya yanaendelea vizuri, kwa upande wetu tuko vizuri kuhakikisha tunapata ushindi wa michuano hii," alisema Semunyu.

Aidha, alisema lengo la mashindano hayo ni kujenga umoja na ushirikiano wa wachezaji kutoka katika klabu hizo na amewashukuru wadhamini wa mashindano hayo Benki ya CRDB kwa kuendelea kuyadhamini mashindano hayo.

Kwa upande wake Katibu wa mashindano Chama cha Gofu Tanzania (TGU), Andrew Sengeu alisema mashindano hayo yatakuza umoja kati ya klabu zinazoshiriki na kusaidia kuendeleza mchezo huo.

# Michezo

Ijumaa Machi 1, 2024

Nipashe




**Ten Hag: Kila ushindi ni muhimu** UKURASA 22



Wachezaji wa Yanga, Aziz Ki (kushoto) na Khalid Aucho wakiwa kwenye mazoezi ya mwisho ya timu hiyo jana kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Cairo kuelekea mchezo wao wa leo wa Kundi A Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly. **PICHA: MTANDAO**

## Benchikha ambadilishia majukumu Kanoute

**Na Saada Akida**

KUELEKEA kwenye mchezo wao wa kesho wa Kundi D Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha wa Simba amembadilishia majukumu kiungo wake Sadio Kanoute na pia ameweka wazi kuwa hawana sababu yakushindwa kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Katika kuhakikisha wanafanikiwa kutengeneza na kutumia nafasi zinazopatikana katika mchezo wa kesho dhidi ya Jwaneng Galaxy, Benchikha amemuandaa Kanoute kucheza nafasi ya mshambuliaji msaidizi akicheza nyuma ya mshambuliaji wa kwanza kutoka kwenye nafasi yake ya kiungo mkabaji.

Kwenye mchezo wa kombe la Shirikisho la FA ambao Simba waliibuka na ushindi wa mabao 6-0 Kanoute alicheza kwenye nafasi hiyo ya nyuma ya mshambuliaji na kufanikiwa kufunga ‘hat trick’.



“Alicheza vizuri sana kwenye nafasi ya mshambuliaji namba 10, anatumia vizuri mipira inayokosewa na mabeki wa upinzani, nadhani atatupa kitu kwenye mchezo dhidi ya Jwaneng galaxy akicheza kwenye nafasi hiyo,” alisema Benchikha.

Alisema mchezo wa Jumamosi ni muhimu zaidi kwao kushinda na ndio sababu ameandaa mbinu tofauti tofauti ili kuhakikisha wanaibuka na ushindi na kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ya Klabu bingwa Afrika.

“Hatuna sababu na hatutakuwa na sababu ya kutoa kama tutashindwa kufuzu, najua mpira una matokeo ya kushangaza lakini tumejiandaa vizuri, ni mchezo muhimu sana kwetu katia safari ya kuingia hatua ya robo fainali,” alisema Benchikha.

ENDELEA UKURASA 23

# Yanga, Al Ahly moto utawaka Cairo

**Na Adam Fungamwango**

### ●●● Kocha Gamondi awataka wachezaji wake kutocheza kwa presha, aahidi soka safi mbele ya...

WAKIWA kwenye kiwango cha hali ya juu kwa sasa, Mabingwa wa Tanzania, Yanga leo watashuka kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Cairo, saa 1:00 usiku (Kwa saa za Afrika Mashariki) kuwavaa mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Al Ahly katika mchezo unaosubiriwa kwa hamu na mashabiki wengi wa soka, huku Kocha Mkuu, Miguel Gamondi akiwataka wachezaji wake kucheza bila presha na kuonyesha soka safi.

**Gamondi amesema hakuna wanachotafuta zaidi ya ‘vita’ ya kuongoza ligi lakini tayari wameshafuzu kucheza robo fainali ya michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi vilabu Afrika.**

Al Ahly ilifanikiwa kutinga hatua hiyo kwa kuifunga Medeama ya Ghana bao 1-0 ikiwa ugenini, huku Yanga ikiitandika CR Belouizdad ya Algeria mabao 4-0 Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Matokeo hayo yamefanya msimamo wa Kundi A kuongozwa na Al Ahly yenye pointi tisa ikifuatiwa na Yanga yenye pointi nane ambazo zote zimefuzu kucheza robo fainali ya michuano hiyo zikiziacha CR Belouizdad na Medeama.

Kuelekea mchezo huo wa leo, Gamondi amesema wamejiandaa kucheza soka safi huku wakiwa na lengo la kusaka ushindi lakini hataki wachezaji wake kucheza kwa presha mchezo huo.

“Ni mechi ngumu, Al Ahly ni timu kubwa na nzuri, ndiyo mabingwa wa Afrika, watakuwa nyumbani kwao mbele ya mashabiki wao, nimewaambia wachezaji wangu tayari tumeshaingia robo fainali, hivyo wasicheze kwa presha na wakifuata nilichowaambia tunaweza kupata kitu hapa Cairo na kuwashangaza wenyeji wetu,” alisema Gamondi.

Alisema itakuwa furaha kwao kama watamaliza mechi zao na kuongoza kundi lao wakishika nafasi ya kwanza.

“Vita ya sasa ni nani atamaliza nafasi ya kwanza na nani atamaliza nafasi ya pili si vita ya kufuzu robo fainali, tumeshapata tiketi hiyo, tutacheza kwa nidhamu huku tukisimamia malengo yetu ya mchezo,” alisema Gamondi.

Alisema Al Ahly watacheza mbele ya mashabiki wao na watataka kupata ushindi ili kuwapa furaha mashabiki wao hivyo watacheza kwa tahadhari kubwa huku wakijipanga kutumia nafasi kwenye makosa watakayoyafanya waarabu hao.

“Itakuwa mechi nzuri sana, ni mechi ya ufundi na kuonyesha kile ambacho kila mmoja anacho,wenzetu watataka kuendeleza matokeo mazuri kwenye uwanja wao wa nyumbani na sisi tunataka kumaliza kwa heshima mechi zetu,” alisema gamondi.

Kwa upande wake, beki wa kati wa timu hiyo, Ibrahim Hamad ‘Bacca’, ameweka wazi kwenye mkutano wa wachezaji ambao haukuwa na kiongozi yoyote wamekubaliana kwenda kupambana kwa sababu’ wanaitaka’ mechi hiyo.

“Tuko vizuri, tumejiandaa vyema kwa ajili ya kupambana kwa ajili ya kupata nafasi ya kwanza, kwa nini tunaitaka ya kwanza, ni kwamba ukiangalia zile timu kubwa, kongwe, ngumu, maarufu na zenye uzoefu zinashika nafasi ya kwanza kwenye makundi, hivyo inakuwa si rahisi sana kukutana nazo za robo fainali, tunaitaka nafasi ya kwanza ya kundi hili tucheze na timu zinazoshika nafasi ya pili kwenye kundi lao,” alisema Bacca.

Alisema mchezo wa leo ni fainali kati yao na Al Ahly ya kuwania nafasi ya kwanza ya kundi hilo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >